Alhamisi Novemba 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581482

nipasheTZ nipasheTZ
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com



**LUKAKU KUBAKIZWA AS ROMA**
UKURASA 21

UKURASA WA 4
**Mke** wa Bilionea Msuya aweka wazi mgawanyo hisa kampuni



UKURASA WA 4
**Hoja** sita Jamhuri rufani kupinga kuachiwa Sabaya



UKURASA WA 5
**Mikopo** makundi maalum yarejea na utaratibu mpya

# Vilevi, kamari, simu msingi Bima ya Afya

• **Asiye** na bima; hapati leseni udereva, pasipoti, laini ya simu, haruhusiwi kidato cha tano, NIDA... *Endelea Ukurasa 2*







## Makonda: Ukiitwa mstaafu pumzika, acha kipaza sauti

UKURASA 3



## ‘Mafao’ wenza wa vigogo yashtua

• **LHRC**, Askofu Munga wang’aka... *Endelea ukurasa 3*

**MICHEZO** SIMBA, YANGA SC HATARI HAPA UK.24 **KATUNI** UK.6

# Pombe kali, vipodozi, michezo kamari sasa kugharimia Bima ya Afya Wote

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imeainisha vyanzo tisa vya mapato vitakavyotumika kupata fedha za kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo jijini hapa jana wakati akiwasilisha bungeni Muswada wa Sheria Na. 8 ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2022 huku akivitaja vyanzo hivyo kuwa ni mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kaboni, vinywaji vikali, bidhaa za vipodozi, kodi ya michezo ya kubahatisha, ada ya bima za vyombo vya moto.

Alivitaja vyanzo vingine kuwa ni mapato yatokanayo na ushuru wa miamala ya kielektroniki kwa kadri itakavyopendekezwa na waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, fedha zitakazotengwa na Bunge, mapato yatokanayo na uwekezaji wa mfuko, zawadi na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali.

Pia alisema kifungu cha saba cha sheria hiyo, kinaainisha majukumu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika kudhibiti na kusimamia mfumo wa bima ya afya nchini.

Alisema kwa mujibu wa kifungu hicho, TIRA pamoja na mambo mengine, itakuwa na wajibu wa kusajili na kudhibiti skimu za bima ya afya, kuhakikisha kuwa kila skimu ya bima ya afya inatoa kitita cha mafao ya huduma muhimu kwa mujibu wa sheria hiyo.

Alisema wajibu mwingine wa TIRA ni kutoa miongozo kuhusiana na uendeshaji wenye tija na ufanisi wa shughuli za skimu za bima ya afya.

## BIMA YA AFYA YA JAMII

Waziri Ummy alisema katika kufikia lengo la Bima ya Afya kwa Wote na kwa kutambua uzoefu na uwekezaji uliofanywa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuanzisha kitita cha Bima ya Afya cha Jamii (CHIP) ikiwa ni mpango mbadala wa CHF ambao sheria iliyoanzisha mfuko huo inapendekezwa kufutwa na kuianzisha upya chini ya sheria hiyo.

"Lengo la kuanzishwa kwa kitita hicho ni kuhakikisha wananchi wote wanajumuishwa katika utaratibu wa bima ya afya ili kupata huduma bora za afya pasipo vikwazo wanavyokutana navyo sasa," alisema.

Waziri Ummy alivitaja vikwazo hivyo ni wananchi kutopata huduma za afya wanapokuwa nje ya maeneo waliojiandikisha na hivyo kulazimu kulipia huduma za afya kwa utaratibu wa papo kwa papo hali inayoathiri shughuli za kijamii na kiuchumi.

Kikwazo kingine, alisema ni wigo mdogo wa kuchangiana kati ya mikoa na halmashauri zenye uchumi mkubwa na mdogo, wananchi wenye kipato kikubwa na kidogo na wagonjwa na wasio wagonjwa kutokana na kusimamiwa katika ngazi za mamlaka za serikali za mitaa.

Alitaja kikwazo kingine kuwa ni ufinyu wa huduma katika kitita cha mafao kinachotolewa, hivyo kukosekana kwa huduma muhimu mathalani huduma za afya ya kinywa na meno, kutojumuishwa kwa baadhi ya dawa na hivyo kumlazimu mwanachama kulipia.

Kikwazo kingine ni muundo wa CHF kutokidhi misingi na kanuni za uendeshaji wa bima ya afya mathalani kutotenganisha kwa majukumu kati ya mnunuzi na mtoa huduma za afya huku akiainisha kwingine kuwa ni uhiari wa wananchi kujiunga unaosababisha wananchi kujiunga wakiwa wagonjwa.

Waziri Ummy pia alisema kifungu cha 21 cha sheria hiyo kinaweka viwango vya uchangiaji kwa wanachama kutoka sekta ya umma, sekta rasmi binafsi na sekta isiyo rasmi.

Alisema serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hicho kwa kubainisha kuwa mchango wa asilimia sita wa mshahara utakuwa kwa ajili ya mwajiri wa sekta ya umma na mwajiri wa sekta rasmi binafsi atakayechagua kuwasajili waajiriwa wake katika skimu ya bima ya afya ya umma.

"Kwa muktadha wa sheria hii mshahara wa sekta ya umma na sekta rasmi binafsi, umetafsiriwa kwa maana sawa na ile inayotumika na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa sekta zote mbili mtawalia. Dhumuni la kifungu hiki ni kuwa na maana zinazofanana na kuhakikisha uwepo wa uwiano katika uchangiaji wa kitita cha mafao ya huduma muhimu," alisema.

## MWANACHAMA KUFARIKI

Ummy alisema kifungu cha 25 kinaweka masharti kuhusiana na ukomo wa uanachama ambapo uanachama utafikia ukomo iwapo mwanachama atafariki au ataacha kuchangia katika skimu ya bima ya afya.

Alisema kifungu kinabainisha kuwa wategemezi wa mwanachama aliyefariki wataendelea kupata huduma kwa kipindi kitakachobainishwa na waziri mwenye dhamana katika kanuni. Lengo la kifungu hicho, alisema ni kulinda haki za wategemezi wa mwanachama.

## UBORA HUDUMA

Waziri Ummy alisema sehemu ya sita inaweka masharti kuhusu udhibiti ubora wa huduma zitolewazo na vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya.

Alisema kifungu cha 26 kina lengo la kuhakikisha skimu za bima ya afya zinazingatia ubora katika utoaji wa huduma za bima ya afya kulingana na miongozo ya TIRA.

Alisema kifungu cha 27 kinaipa Wizara ya Afya jukumu la kuhakikisha kuwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya za umma na binafsi vinatoa huduma bora za afya kwa wanufaika kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyotolewa na wizara.

## UDANGANYIFU

Waziri Ummy alisema kifungu cha 34 cha sheria hiyo kinaweka katazo kwa wanufaika, vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya na mtu yeyote kutoa taarifa za uongo na kuweka adhabu iwapo watathibitika kufanya hivyo.

Alisema dhumuni la kifungu hicho ni kulinda uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya kwa kuzuia masuala ya udanganyifu na ubadhirifu wa pesa za wanachama ili kuhakikisha huduma za bima ya afya zinazotolewa zinakidhi vigezo na ni endelevu.

## ADHABU WASIOJIUNGA

Kwa mujibu wa Ummy, serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuweka adhabu ya asilimia 10 ya mchango wa kila mwaka kwa mtu yeyote ambaye hatajiunga na bima ya afya kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuanza kutekelezwa kwa sheria inayopendekezwa.

Alisema hata hivyo waziri amepewa mamlaka ya kutoa msamaha wa ulipaji wa adhabu ya asilimia 10 kwa kuzingatia maslahi ya umma au sababu nyingine yoyote.

Kuhusu ushiriki wa sekta binafsi kwenye bima ya afya kwa wote, Waziri Ummy alisema sheria inaeleza kwamba kutakuwa na utaratibu wa kampuni binafsi kusajiliwa kama skimu za bima ya afya binafsi baada ya kutimiza vigezo na masharti yatakayoainishwa katika kanuni zitakazotungwa chini ya sheria inayopendekezwa.

Alisema lengo la kifungu hicho ni kuwawezesha wananchi kuwa na uhuru wa kuchagua aina ya skimu ambazo watapenda ziwahudumie na kupanua wigo wa uwepo wa skimu za bima ya afya ili kuongeza fursa ya ushiriki kwa lengo la kukuza ushindani na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za bima ya afya nchini.

## ANGALIZO LA WABUNGE

Katika hilo wabunge wametoa angalizo kwa serikali kutumia mfumo mzuri wa kuwatambua wananchi maskini na wasiojiweza watakaopata huduma ya bima ya afya kwa wote bure, ili kuunusuru mfuko huo kufilisika.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Bernadeta Mushashu, alisema: "Ibara ya sita ya muswada wa sheria hii inamtambua watu wasiokuwa na uwezo ili wapate matibabu pasipokuwa na fedha.

Sensa ya Watu na Makazi imeshaeleza idadi kwa wananchi wasio na uwezo ni 15,800,756 sawa na kaya 3,637,121. Aidha wananchi wasio na uwezo na ambao wanaishi katika umaskini uliokithiri ni 4,044,843 ambao ni asilimia nane sawa na kaya 1,113,513."



"Naweka angalizo hapa mkisema kila mtu maskini akapate matibabu bure kila mtu atakwenda. Tuwe waangalifu, tuweke vigezo mahususi vya kumfumbua mtu asiye na uwezo, huu mfuko utaelemewa na utakufa tusipokuwa makini".

Kadhalika, alisema wakati serikali inawatambua watu wasio na uwezo na maskini basi watu wenye ulemavu nao watambuliwe katika makundi hayo.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacquline Kainja, aliipongeza serikali kwa kutafuta vyanzo vya mapato vya kuendesha Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote lakini akaishauri serikali namna ya kuwapata wananchi wasiojiweza, kwamba utumike utaratibu mzuri wa kuwapata watu wasiojiweza.

Akitolea mfano, Kainja alisema hata Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao bado unachangamoto katika baadhi ya maeneo, akiomba uboreshwe kwa sababu serikali huenda ikatumia mfuko huo katika kuwapata walengwa.

Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima , alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wa kuanzisha bima ya afya kwa wote. Alisema asilimia tano ya Watanzania hawawezi kupata huduma ya afya kutokana na vikwazo vya fedha walivyo navyo.

"Hatuwezi kuchelewa hata dakika moja kuupitisha muswada huu. Wananchi wetu ni maskini sana, wengi wanapoteza maisha kwa magonjwa yanayoweza kutibika. Walio na uwezo walipe bima ili kuwabeba wagonjwa," alisema Gwajima huku akishauri maeneo ya vijijini yasiyo na zahanati zijengwe ili wananchi wapate sehemu ya kupata matibabu.

Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Francis Mtinga, aliishauri serikali kuajiri watumishi wa afya wengi ili waende kwenye vituo vya afya ili suala la utekelezaji wa bima ya afya kwa wote lifanikiwe.

Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndugulile alisema: "Tukumbuke afya ina mihimili minne, elimu ya afya, kinga, tiba na huduma za utengamaa. Sisi tunaangalia tiba tu. Sasa tunahama kutoka kwenye magonjwa ya kuambukiza kwenda kwa yasiyoambukiza".

Hata hivyo aliishauri serikali kuweka mifumo mizuri ya uendeshaji na usimamizi wa bima, kutoa elimu pamoja na kutenga bajeti ya kutosha ya kutekeleza uhamasishaji wananchi ili waweze kuelewa.

"Tuwekeni motisha kwa nini mtu ajiunge na bima ya afya, nimeona mmeweka adhabu. Mfano mtu asiye na bima gharama yake iwe juu lakini mwenye bima iwe nafuu, hii itamvuta mtu kukata bima," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christina Mzava, alisema bima ya afya ni takwa la kikanda na kimataifa na haki ya kila Mtanzania.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
02.11.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 04-11-2023 hadi 09-11-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Geita kwenda Dar-Es-Salaam,** gari ilo lina namba ya usajili: **T 454 DYG / T 153 CHN**
2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 4.20**
   **Kimo - mita 5.20**
3. Njia itakayotumika: **Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Morogoro, Pwani mpaka Dar es salaam** kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Makonda: Ukiitwa mstaafu pumzika

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, amesema kiongozi akiitwa mstaafu ni vyema kupumzika, akikosoa alichokiita 'kila siku kwenye kipaza sauti'.

Jijini hapa jana baada ya kupokewa na wanachama na wafuasi wa CCM wa Mkoa wa Dodoma, Makonda alisema: "Ukiitwa mstaafu tulia, lea familia yako. Wakikuona wa maana watakuita kama walivyomwita Makonda, huwezi kuwa mstaafu halafu kutwa kwenye kipaza sauti.

"Wastaafu wa nchi hii wanaheshimika sana na mimi nimejifunza kutoka kwao. Kuna siku nilikwenda kwa Mzee Mkapa, nikamwambia 'upo kimya sana'. Akaniuliza 'unataka nifanye nini?' Akasema 'mimi nimemaliza wajibu wangu. Kwahiyo, mimi ninaamini kazi yetu kubwa ni kumtia moyo Rais wetu ni kumsaidia na kuwalinda viongozi wetu, tuache wafanye kazi'. Kuna watu tunawajua wanawalipa watu wachafue viongozi mtandaoni," alidai.

Alitoa rai kwa viongozi wa vyama vya upinzani kama kuna taarifa wangependa CCM izifanyie kazi, watoe taarifa, ikiwezekana kwa wazee wa chama hicho.

"Tunajenga nyumba moja, mkiwa na taarifa muhimu na mahsusi kaka zangu Mbowe, Tundu Lissu na Lema, mtoe taarifa hata kama mimi mnaniogopa kunipa, basi tuna wazee kina Kimbisa waambie CCM liangalieni hili kwa maslahi ya taifa," alisema.

### PM APEWA MIEZI 6

Makonda pia alisema CCM imetoa miezi sita kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kusimamia kikamilifu utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji kwa Sekretarieti ya CCM.

Makonda alisema amepewa jukumu la kusema na si kupamba watu na atasema kero za wananchi na si kuwapa watu sifa wasizostahili.

### SILAA MIEZI MIWILI

Kuhusu Dodoma, Makonda alisema wananchi wa hali ya chini na wamiliki wa ardhi Jiji la Dodoma walipokea ujio wa makao makuu kwa furaha na wananchi wa mikoa mingine waliamua kununua ardhi mkoani Dodoma, lakini dhuluma inalia kwenye jiji hilo.

"Dhuluma hii inafanya wananchi wa Dodoma kutamani kujiua, maelekezo ya CCM kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ninakupenda na kuheshimu lakini nilipo si matakwa yangu tena, ni ya CCM, chama kinakupa miezi miwili kuanzia leo tusisikie mwananchi wa Dodoma analia juu ya ardhi yake.

"Januari Mosi 2024, wananchi wa Dodoma wanakwenda kula mwaka mpya hawana migogoro ya ardhi, Jerry umeanza vizuri na ninakuahidi una ushirikiano wa CCM na kama kuna kigogo yeyote amedhulumu ardhi ya maskini na mnyonge, ardhi hiyo ataitapika.

"Kama kuna mtumishi anashirikiana kudhulumu na kumnyima haki mwananchi kisa hana ndugu, ndugu yake ni CCM tutasema kwa niaba yake," alitamba.

### KWA MAWAZIRI

Makonda pia alisema CCM inawaagiza mawaziri kuhakikisha kila robo ya mwaka ya kibajeti wanaandaa taarifa na kuiwasilisha sekretarieti ya CCM Taifa ikielezea utekelezaji kazi waliyopewa na serikali.

"Kazi wamepewa na mwenyekiti wa chama na chama kinataka ripoti, waziri yeyote atakayekaa ndani ya robo ya mwaka hajafanya kazi, hana ripoti, hakuna utekelezaji wa ilani chama hakitasita kumchukulia hatua kwani sasa ni wakati wa kufunga mkanda kuwatumikia wananchi," alisema.

Aliwaagiza makatibu wote wa CCM nchi zima watoe taarifa za viongozi wa serikali wanaokwenda kwenye mikoa bila kuripoti kwenye ofisi za CCM.

Makonda alisema Dodoma ndio makao makuu, lakini upatikanaji wa maji ni asilimia 51, akifafanua: "Tunataka Jiji la Dodoma yapatikane maji ya kutosha, nimeambiwa upo mpango wa uchimbaji visima ambao ni wa muda mfupi na upo wa muda mrefu.

"Rai yangu kila anayehusika aifanye kazi kikamilifu, katika kutoa taarifa ya utekelezaji wa ilani kwa sekretarieti yetu. Tunataka kuona maji ni kipaumbele kwa Jiji la Dodoma."




Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, akitumia usafiri wa bajaji alipowasili katika halfa ya mapokezi yake kwenye viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Malipo ya fadhila wenza wa vigogo yashtua

**Na Waandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ametoa angalizo katika vifungu vya sheria vinavyohusu malipo ya fadhila kwa wenza wa viongozi wastaafu, akitoa ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Dk. Eliezer Feleshi kutupia jicho baadhi ya maeneo ili yasilete mkanganyiko katika jamii.

Juzi Bunge lilipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambao pamoja na mambo mengine, unaweka malipo ya fadhila kwa wenza wa viongozi wastaafu ambao ni Rais mstaafu, Makamu wa Rais mstaafu na Waziri Mkuu mstaafu.

Baadhi ya vifungu vilivyoongezwa ni 9A,12A, 14A ambavyo vinawawezesha wenza wa viongozi hao kulipwa kiinua mgongo wakati wa kipindi cha uongozi wa wenza wao.

Baada ya muswada huo kupitishwa juzi usiku, Dk. Tulia alisema mtu hawezi kupokea mafao mara mbili kwa wakati mmoja akiwa serikalini.

Hivyo, alitoa ushauri kwa AG kuangalia sehemu hiyo kwa kuweka maelezo kwamba atapata stahiki hizo ikiwa hafanyi kazi ama ameacha kazi.

Dk. Tulia alisema itakuwa vigumu kwa mwananchi kufahamu (mwenza) kama bado anafanya kazi na bado ni mwenza wa kiongozi atalipwa mara moja kwa sababu bado anatumikia kazi yake.

Vilevile, Dk. Tulia alitoa angalizo la kuangaliwa kwa muda ambao kiongozi amefanya kazi na malipo anayostahili kulipwa, akisema (kiongozi) anaweza kufanya kazi kwa muda wa mwezi mmoja na kwa mujibu wa marekebisho ya vifungu hivyo atastahili kulipwa mafao.

Dk. Tulia alisema: "Ni lazima kutazamwa hili kwa sababu hata yale mafao ya kawaida ya watumishi wanayolipwa huwa ni lazima kuwe na muda ambao amefanya kazi. Hivyo (AG) ni vyema kutazama haya mafao ya viongozi awe amefanya kazi kwa muda gani, Je, yatafanana au yatakuwa tofauti?" Aliagiza.

### USHAURI WA KAMATI

Akisoma maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Florent Kyombo, alisema katika marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, inayolenga kuweka malipo kwa wenza wa vigogo wastaafu ni vyema serikali ikaondoa maneno kiinua mgongo na kuandika malipo ya fadhila.

Alisema kamati inapendekeza kuondoa maneno hayo kwa kuwa muktadha wa sheria hiyo yanatumika kuwalipa watumishi wa umma.

### WADAU WASHTUKA

Wanasheria, viongozi wa dini na wanasiasa wamesema kitendo cha wenza wa viongozi kupewa malipo hayo ya fadhila kinasababisha mzigo mkubwa kwa taifa na kuleta matabaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, akitoa maoni yake jana kuhusu suala hilo, alisema uamuzi huo ni mzigo kwa taifa na usio na sababu kwa kuwa mpaka sasa ipo mingi.

"Ni sawa na kumpa mshahara mtu asiyefanya kazi. Pensheni ni mshahara umeufanyia kazi, nguvu zimeisha unaendelea kulipwa kwa kuwa umefanya kazi ya kujenga taifa. Huyu ambaye ni mwenza wa kiongozi amefanya kazi gani?" alihoji.

Dk. Anna ambaye kitaaluma ni mwanasheria, aliongeza: "Amefanya kazi ya kupikia familia yake, sawa. Kwahiyo, kama ni kupikia familia yake waboreshe sheria ya mirathi na mambo mengine ya kifamilia, siyo wananchi kubebeshwa mzigo kuwatunza tena wenza wao. Mwingine ana wake wanne kwa maana wote watafanyiwa hivyo, hii ni changamoto kubwa."

John Mrema, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), aliitafsiri ni sheria mbaya na kandamizi. Inajenga matabaka katika taifa. Inakinzana na Katiba ya nchi inayokataza kuwapo sheria zenye kujenga matabaka.

"Wenza hawa wanalipwa kwa sababu tu walibahatika kuwa wenza na si kwamba kuna kigezo kingine chochote kile. Viongozi wa nchi hii ni wengi. Kwanini sheria hiyo iseme ni kwa viongozi wakuu tu na ambao wanalipwa mafao makubwa kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya Viongozi?

"Sheria hiyo ya mafao ya viongozi inatamka kuwa hata ikitokea kiongozi amefariki (dunia), mwenza wake ataendelea kulipwa mafao hayo mpaka mwisho wa maisha yake na atakuwa analipwa asilimia 80 ya malipo ya kiongozi aliyeko madarakani," alisema.

Mrema alisema sheria hiyo haifai ikizingatia Bunge hilo hilo limetunga sheria aliyoiita kandamizi ya kikokotoo kwa wastaafu wengine katika taifa.

Naye Askofu mstaafu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Stephen Munga aliandika katika ukurasa wake wa Facebook jana: "Hivi ni kweli Bunge linalowakilisha walalahoi ndiyo limepitisha hii?

"Kweli siamini! Hii si sawa. Hii si haki. Yaani kodi za walimamihogo zikalipe mafao ya wenzi wa wakubwa? Hivi matatizo ya Watanzania yameisha kiasi kwamba tuna ziada ya kufuja? Jamani kuweni na huruma ninyi kwa ninyi."

Nipashe ilijiridhisha kuwa ujumbe huo aliandika Askofu Munga baada ya kumpigia simu kiongozi huyo wa kiroho jana jioni.

HABARI KITAIFA

# Hoja sita Jamhuri rufani kupinga kuachiwa Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JAMHURI imewasilisha hoja sita katika Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Arusha, kumwachia huru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai ole Sabaya.

Hoja hizo ziliwasilishwa jana na mawakili wa serikali mbele ya jopo la majaji wa mahakama hiyo lililoketi mkoani hapa chini ya Jaji Jacobs Mwambegele.

Mei 6, 2022, Mahakama Kuu Masjala ya Arusha, chini ya Jaji Sedekia Kisanya, ilimwachia huru Sabaya na wenzake baada ya kuhukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Arusha kifungo cha miaka 30 jela Oktoba, 2021. Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Odira Amworo, baada ya kutiwa katika kesi namba 105 ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine walikuwa Sylvester Nyegu na Daniel Mbura. Wote walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Wakili Mkuu wa Serikali, Sabina Silayo, aliwasilisha hoja hizo kwa upande wa Jamhuri akisaidiana na Eliainenyi Njiro, Chivanenda Luwongo na Verediana Mlenza. Mawakili wa wajibu rufani ni Mosses Mahuna, Fauzia Mustapha, Sylvester Kahunduka na Fridolin Bwemelo.

Akiwasilisha hoja hizo, Wakili Mkuu Silayo, alidai kuwa wametoa sababu sita kwa nini hawakuridhika na uamuzi wa Mahakama Kuu wa kutengua hukumu ya mahakama ya chini.

Katika hoja ya kwanza na ya sita, wataziacha kama zilivyokuwa na hoja ya tatu, nne na tano, waliomba kuzikusanya kuwa pamoja ila ya kwanza waliondoa.

Alidai kuwa hoja ya sita baada ya kupitia uamuzi wa Mahakama Kuu, Jaji alisema shahidi wa pili wa warufaniwa hakupewa haki ya kuuliza maswali ya dodoso kwa mashahidi wa kwanza na wa pili wa waleta rufani.

Hata hivyo, alidai kuwa wameona kuwa Jaji hakujielekeza na ombi hilo kwa kuwa shahidi wa mrufani wa kwanza alipewa haki yake ya kuuliza maswali. Pia alidai kuwa Jaji wa Mahakama Kuu hakuwa sahihi kwa kusema hati ya mashtaki ilikuwa na mashtaka matatu na kila kosa lilitakiwa kuwa kivyake.

Alidai kwa hoja ya kwanza, kwa kuwa mrufani alipewa haki yake pia kwa hoja ya pili hati ya mashtaka ilikuwa na makosa matatu na kila kosa lilikuwa linaweza kusimama lenyewe.

"Hoja ya tatu si ushahidi wa shahidi wa pili uliotumika tu kuwatia hatiani kwa kuwa mashahidi wengine walipata haki, hivyo Mahakama Kuu haikuzingatia ushahidi wa wengine ambao uliwatia hatiani. Kwa kuwa si ushahidi wa shahidi mmoja uliotumika kuwatia hatiani, ni maombi yetu Mahakama ya Rufani itakubaliana na rufani yetu," alidai.

Pia alidai kuwa wakati mahakama ya chini ikitoa hukumu, ilijikita zaidi kwa kuunganisha ushahidi wa shahidi wa pili na wa nne wa waleta rufani.

Kwa hoja ya kwanza, alidai wanalalamikia uamuzi wa Jaji kwa kuwa kwa mujibu wa sheria, kuna utaratibu ambao unazingatia mambo matano ikiwamo kama mshtatiwa hatakuwapo mahakamani lakini ana mawakili baada ya maelezo ya awali hakuna shida.

Utaratibu wa pili, alidai kuwa inawezekana mahakama kumuuliza maswali shahidi kwa njia ya kiapo au la na kwamba baada ya hapo mahakama kuorodhesha mambo kutoka pande zote na baada ya kuorodhesha.

Naye Wakili Njiro alieleza sababu ya tatu kwa kugusia vipengele vitatu, cha kwanza kikiwa mahakama ya kwanza ilivyowatia hatiani ilikuwa sahihi. Alidai katika hati ya mashtaka, ukurasa wa kwanza na pili walishtakiwa kwa makosa matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha lakini walihukumiwa kwa kutumia silaha lakini mahakama kuu ilitoa hukumu.

"Ukurasa wa 1099 wa rekodi za mahakama pia paragrafu ya tatu upande wa mleta rufani, tunafananisha hii sawa na mahakama ya kwanza, hivyo tunaomba ulifanyie kazi.

Sisi tunaona haikuwa sawa kutoa hukumu kutoka kwenye unyang'anyi wa silaha kwenda kwa uhalifu wa kikundi.

"Pili, kuna mkanganyiko wa ushahidi kwa kuwa Jaji alisema hakukuwa na ushahidi usioacha shaka na ushahidi wa mashahidi ulikinzana. Katika kosa la pili, Jaji haikutaja lesoni na waleti na mahakama ilisema hayo katika hukumu yake ya 1224 baada ya kusema hivyo. Kwa upande wetu, tunaona si sahihi kwa kuwa katika kosa la kwanza fedha zilizoibwa zilikuwa ni Sh. 2,769000 .

"Kosa la pili, ziliibwa Sh.390,000 na pia ukiangalia katika ushahidi uliotolewa, wako mashahidi walioieleza makama kuwa kuna waleti iliyoibwa pamoja EFD. Tunakubali kulikuwa na utofauti kwenye ushahidi na hati ya mashtaka lakini haijadhuru vyovyote warufaniwa kwani viini vya unyang'anyi kwa kutumia silaha vilithibishwa.

"Japokuwa tumezungumzia suala la mrufani wa pili kutokuwa haki ya kuuliza maswali ya dodoso, warufani wengine walipata nafasi hiyo. Mheshimiwa Jaji tunaona kwamba warufani walikwenda dukani pale kwa ajili ya upekuzi lakini ukiangalia kwa kina, walijificha kwenye kivuli hicho kwa kuwa walitenda uhalifu kwa kupiga watu na kuwachukulia simu na fedha zao," alidai.

Aliendelea kudai kuwa: "Mkanganyiko wa tatu katika hukumu iliyotolewa na mahakama ya chini inahusiana na kamera ya CCTV katika eneo la tukio, hazikuwa nzuri kwa ajili ya kutimiwa ndiyo maana hazikuletwa hivyo tunaona Jaji alijielekeza vibaya.

"Mfano shahidi namba nane alieleza mahakamani kuwa kulikuwapo na CCTV nne ambazo zilikuchua tukio kwenye maeneo tofauti ndani ya duka lakini picha zile hazikufaa kwa ajili ya kutumia. Tunaomba hii kupitia na kuchambua ushahidi huu kwa makosa matatu na kukubaliana na uamuzi wa mahakama ya awali," alidai.

Naye Mosses Mahuna, akijibu kwa niaba ya wajibu rufani wote, alidai kuwa hoja ya kwanza na ya sita, wameelewa kwamba ni haki ya mtu kupewa nafasi ya kuwafanyia ila mrufani wa kwanza na pili hawakupewa nafasi ya kuuliza maswali kwa kuwa ilikuwa haki yao kusikilizwa na kuuliza maswali ya dodoso kwa mashahidi wa Jamhuri wa kwanza na wa pili hakuwatia hatiani na kwa muktadha huo jaji alikuwa sahihi.

Alidai kwa hoja ya tatu imebeba hoja nyingine ikiwamo ya kwanza, hivyo kwa kuwa walipaswa kufanya mabadiliko ya hati ya mashtaka, hivyo Jaji wakati akitoa uamuzi, aliona kulikuwa na makosa katika ya hati ya mashtaka.

"Kulikuwa na makosa kwenye kiasi halisi cha fedha kilichochukuliwa na waleti, lesoni na eneo la duka ambalo limeelezwa liko bondeni ilihali liko soko kuu Arusha. Kosa hili la unyang'anyi wa kutumia sihala litaweza kuthibitika vipi ilihali kuna makosa yaliyojitokeza katika hati ya mashtaka?

"Katika ushahidi mzima hakuna kokote tumeambiwa aliyeiba Sh. 2,769,000 kwa kuwa siku ya tukio haikujulikana kama pesa zimechukuliwa hadi baada ya siku tatu kupita. Katika ushahidi wa mashahidi wote, hakuna aliyesema silaha ilitumika kuchukua vitu au kuiba," alidai.



Jaji Mwambegele, baada ya kusikiliza hoja za pande zote, alisema uamuzi wa rufani hiyo utaandikwa na utasomwa na Msajili kwa tarehe itakayopangwa.

# Mke wa Bilionea Msuya abainisha mgawanyo hisa

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA mke wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya, maarufu Bilionea Msuya, Miriam Mrita, ameieleza mahakama kuwa katika mgawanyo wa hisa kwenye kampuni mbili za marehemu mume wake, hakuna jina la Miriam Steven Mrita bali kuna jina la Miriam Erasto Msuya.

Aidha, amedai kuwa anakubali kwamba taarifa mbalimbali za Jeshi la Polisi zinatoka kwa raia na Ndeshukurwa (mama mkwe wake) ni raia wa Tanzania.

Mrita alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akijibu maswali ya dodoso kutoka kwa Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, kuhusiana na tuhuma za mauaji ya wifi yake, Aneth Msuya.

Wakili Kimweri aliendelea kumuuliza mshtakiwa maswali mbalimbali yaliyotokana na ushahidi wake alioutoa mahakamani dhidi ya tuhuma za mauaji huku akidai mama akimuua mwanawe au mtoto akimuua mzazi wake, lazima kuwapo na sababu.

**Kimweri:** Wewe na Aneth ni mtoto wako wa kumzaa?

**Mrita**: Si wa kumzaa.

**Kimweri:** Kwa hiyo utakubaliana na mimi kwamba kulea au kumzaa mtoto huwezi kuwa na sababu ya kumuua.

**Mrita:** Kutakuwa na sababu ya mauaji.

Kimweri: Mzazi au mlezi anaweza kuwa na sababu ya kuua.

**Mrita:** Ndiyo.

**Kimweri:** Shahidi unakumbuka juzi nilianza kwa kukuuliza majina yako na pia hata wakati unaapa ulitaja majina gani.

**Mrita:** Miriam Steven Mrita.

**Kimweri:** Uliieleza mahakama kama una majina mengine tofauti na Miriam Steven Mrita.

**Mrita:** Sikuiambia.

**Kimweri:** Katika ushahidi wako uliieleza mahakama kwamba ulikuwa mwanahisa kwenye kampuni za Erasto Msuya. Sasa mimi nakuuliza swali kupitia kielelezo DE 6, tuambie majina ya wanahisa yaliyoandikwa hapa, nisomee ukurasa wa 21.

**Mrita:** Erasto Elisaria Msuya na Miriam Erasto Msuya.

**Kimweri:** Jina lako ulilojitambulisha mahakamani na jina lililoandikwa kwenye kielelezo hicho unavyoona yanafanana yaani Miriam Steven Mrita na Miriam Erasto Msuya?

**Mrita:** Jina la Steven ni la baba yangu mzazi.

**Kimweri:** Miriam Steven Mrita na Miriam Erasto Msuya yanafanana?

**Mrita:** Ndiyo.

**Kimweri:** Kwa mujibu wa hiyo nyaraka mgawanyo wa wanahisa, Miriam Steven Mrita hana hisa. Kuna hisa 400 za Erasto Msuya na hisa 200 za Miriam Erasto Msuya. Sasa ieleze mahakama huyo Miriam Mrita ana hisa?

**Mrita:** Hana mheshimiwa.

**Kimweri:** Nitakupeleka kwenye ukurasa wa mwisho wa kielelezo chenu. Nataka uiambie mahakama kuna jumla ya hisa ngapi zilizogawanywa ni 300,000,000 katika hisa 3000 kila hisa ni Sh. 100,000 lakini kabla ya kwenda huko utakubaliana na mimi kwamba ndiyo inayosomeka hapo?

**Mrita:** Ndiyo.

**Kimweri:** Nitakupeleka kwenye ukurasa namba 21 ni hisa ngapi hapo.

**Mrita:** Erasto hisa 600 na Miriam Erasto Msuya hisa 200. Jumla ni hisa 800

**Kimweri:** Nakupeleka kwenye kielelezo DE 7 ambayo ni nyaraka ya kampuni ya Unique Mining Limited, angalia halafu uileze kama wewe Miriam Steven Mrita jina lako lipo hapo.

**Mrita:** Hakuna.

**Kimweri:** Mheshimiwa Jaji nitamwelekeza kwenye ukurasa wa nane, hisa zilizogawanywa kwa wanahisa ni hisa ngapi?

**Mrita:** Ni hisa 1,000.

**Kimweri:** Hisa za jumla za kampuni ni hisa ngapi zilizogawanywa kwa wahusika.

**Mrita:** Erasto 400, Miriam Erasto Msuya 100.

**Kimweri:** Hao wanaomiliki waligawana hisa ngapi.

**Mrita:** Hisa 500.

**Kimweri:** Unakubaliana na mimi kwamba taarifa mbalimbali za Jeshi la Polisi pia wanazipata kutoka kwa raia? Kwa sababu kwenye ushahidi wako ulishangaa sana mama wa nyumbani kutoa taarifa kwa jeshi hilo.

**Mrita:** Ndiyo.

Kimweri: Huyu Ndeshukurwa ni raia wa Tanzania?

**Mrita:** Ndiyo.

**Kimweri:** Sasa ulikuwa unashangaa nini Ndeshukurwa kuwapa taarifa Jeshi la Polisi alipokuwapo Getruda Mfuru dada wa kazi wa Aneth.

**Mrita:** Ni kweli nilishangaa.

**Kimweri:** Kwa unavyodhani wewe kuna muda wa mtu kukaa na kitisho ndani yake.

**Mrita:** Sijui.

**Kimweri:** Sasa ulishangaa nini kama hujui ni muda gani, kwa sababu katika ushahidi wako hapa ulishangaa sana Getruda Mfuru kukaa na kitisho ndani yake.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi leo. Upande wa utetezi katika kesi hiyo utaendelea kutoa ushahidi wake.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni, Dar es Salaam, alikiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo. Mshtakiwa wa Pili, anaitwa na Revocatus Muyela.

## HABARI KITAIFA

# Utaratibu mpya mikopo kwa makundi maalumu katika hatua za mwisho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho za kuja na utaratibu mpya wa kutoa mikopo kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mapema mwaka huu, serikali ilitangazwa kusitishwa kwa utoaji mikopo hiyo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na kuahidi kuja na utaratibu mpya ili kuondokana na matatizo yaliyojitokeza awali.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Festo Dugange (pichani), aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nanyumbu (CCM), Ally Mhata.



Katika swali lake la nyongeza, Mhata alisema serikali imesitisha utoaji mikopo ili kupisha kuanza utarajibu mzuri.

"Je, serikali haioni haja ya kuja na mpango wa dharura wa kutoa mikopo kwa sababu wananchi wanahitaji hasa kipindi cha kilimo?" alisema.

Dk. Dugange alisema lengo la serikali kutoka fedha hizo kwa makundi hayo ni kuwa ziwafikie walengwa, zitumike kwa tija na zikusanywe ipasavyo.

"Serikali inaendelea kwa kasi na suala hilo ili kuanza kutoa mikopo badala ya kuwa na mpango wa dharura ambao utakuwa na mapengo. Hivyo muda si mrefu mikopo hiyo itaanza kutolewa kwa utaratibu mzuri," alisema.

Katika swali la msingi, Mhata alitaka kujua ni lini serikali italeta sheria ya kuruhusu halmashauri kutumia benki kama wakala wa ukopeshaji na ukusanyaji madeni.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema serikali inatambua ufanisi wa kutumia benki kama wakala huo kwa kuzingatia kuwa benki zina miundombinu na utaalamu wa kutoa huduma hizo.

Hata hivyo, alisema ili kutumia benki katika kutekeleza jukumu la mikopo ya asilimia 10, maandalizi na utafiti unapaswa kufanyika ili kuendana na lengo kusudiwa.

Awali, alifafanua Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliunda Kamati ya Kitaifa ambayo ilichambua na kuandaa mapendekezo ya uendeshaji wa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri na timu imeshakamilisha kazi hiyo na kuwasilisha maoni na mapendekezo na serikali inaendelea kufanyia kazi na baada ya kukamilisha itatoa utaratibu.

## Wawili wafa maji, watano hawajulikani boti ikizama

**Na Julieth Mkireri,** MAFIA

WATU wawili wamefariki dunia na wengine watano hawajulikani waliko baada ya boti waliyokuwa wakisafiria kutoka Mafia kwenda Kibiti, mkoani Pwani kuzama Mto Rufiji.

Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Zephania Sumaye, alisema tukio hilo lilitokea Jumatatu saa nane mchana baada ya boti hiyo ya wavuvi kudaiwa kugonga kingo za mto huo.

Sumaye alisema boti hiyo ilikuwa na wavuvi 15, kati yao wanane wameokolewa wakiwa hai na wawili wakiwa wamekufa na watano hawajapatikana.

Alisema miili ya watu waliopolewa jana ni mwanamume ambaye hajafahamika jina lake na Mwanahamis Hamis (28), mkazi wa Bungu, Kibiti.

Alisema jitihada za uokozi zinaendelea kufanywa na timu ya uokoaji ambayo imejipanga baada ya tahadhari zinazoendelea kutolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kutokana na mvua kubwa kunyesha Mafia, likiwa ni moja ya maeneo yaliyotajwa kupata mvua.

"Mamlaka imetoa tahadhari na sisi tunaendelea kuwasisitiza wakazi wa Mafia na wanaozunguka Bahari ya Hindi kuwa makini katika kipindi hiki kwa kuzingatia tahadhari zinazotolewa," alisema.

Sumaye alisema wavuvi na watu wengine wanaofanya shughuli zao kando ya Bahari ya Hindi wanatakiwa kuzisitisha kwa muda ili kuepuka madhara.

Juzi, TMA ilisisitiza uwapo wa mvua za El-Nino na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari kukabiliana na athari.

Pia, ilitabiri uwapo wa mvua za wastani mpaka juu ya wastani kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka ambayo ni Kigoma, Rukwa, Katavi, Tabora, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma na eneo la Kusini mwa Mkoa wa Morogoro.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ichukuliwe kwa mvua zilizoanza kunyesha

**MAMLAKA** ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), juzi ilitoa utabiri wa uwapo wa mvua za wastani mpaka juu ya wastani katika maeneo mbalimbali nchini huku ikibainisha kuwapo kwa uwezekano wa kunyesha mvua za El-Nino, hivyo kuwataka wananchi kuchukua tahadhari kukabiliana na athari zinazoweza kutokea.

Katika taarifa hiyo ya utabiri, TMA ilisema mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka ambayo ni Kigoma, Rukwa, Katavi, Tabora, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma na eneo la Kusini mwa Mkoa wa Morogoro inatarajia kupata mvua za wastani wa juu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kipindi cha nusu ya msimu ambacho ni Novemba hadi Januari, mwakani, kinatarajiwa kuwa na mvua nyingi kulinganisha na nusu ya pili ambayo ni Februari hadi Aprili, 2024) na kwamba katika mvua hizo, kunatarajiwa pia kuwapo kwa El Nino.

Kuwapo kwa mvua hizo kubwa, kwa mujibu wa TMA, kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo athari mbalimbali kama vile uharibifu wa mbiundombinu, mafuriko kuongezeka kwa kina cha maji katika mito na mabwawa unyevu uliopitiliza katika mazao. Hatua hiyo inaweza kusababisha maafa kwa binadamu na mali zao.

TMA katika taarifa hiyo ya utabiri, ilisema mvua hizo zilitarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi uliopita na ni kweli baadhi ya mikoa kuna ripoti za kuanza kwa mvua ambazo zimeanza kuonyesha dalili za kuwapo kwa maafa. Katika maeneo ya kaskazini hususan Tanga, imeelezwa kuwa mvua kubwa zilinyesha usiku wa kuamkia jana na kusababisha changamoto ya usafiri.

Aidha, kama ilivyotabiriwa, mkoa wa Dar es Salaam pia mvua zilianza kunyesha tangu usiku wa kuamkia jana kwenye maeneo mbalimbali. Hizo ni ishara kwamba wananchi katika maeneo mbalimbali wanatakiwa kuchukua tahadhari kuhusu mvua hizo ili kujikinga na majanga yanayoweza kujitokeza wakati wowote.

Licha ya mikoa ya Pwani na Kanda ya Kaskazini, katika mikoa ya Kanda ya Ziwa mvua zimeshaanza kunyesha huku ikibainishwa kuwa ongezeko la mvua linatarajiwa kuwa kubwa kuanzia sasa hadi Novemba. Hata hivyo, kwa Kanda ya Ziwa mvua zilishaanza kunyesha na kuna baadhi ya maeneo kumejitokeza maafa yakiwamo watu kukosa makazi huku nyumba za ibada na majengo ya shule yakiharibiwa hususan katika mkoa wa Kagera.

Kuna msemo kwamba mdharau mwiba mguu huota tende. Msemo huu unasadifi na majira haya kutokana na mamlaka husika katika masuala ya majanga kutangaza viashiria vya kuwapo hatari ya kutokea maafa lakini watu wamekuwa wakishindwa kuchukua hadhari.


Tayari TMA imeshatangaza kuwapo kwa mvua kubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwamo mvua za El Nino lakini baadhi ya watu wanabeza kuwa huo ni utabiri tu. Sasa mvua zimeanza kunyesha katika maeneo mbalimbali, hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuchukua hatua dhidi ya hatari na maafa vinavyoweza kutokea kutokana na mvua hizo.

Jambo la muhimu ni kwa mamlaka husika kwa kushirikiana na wananchi kuhimiza usafi wa mazingira ikiwamo kuzibua mafereji inayopitisha maji ili yapite kwa urahisi bila kikwazo na wakati huo huo, watu waishio mabondeni ambao hukumbwa na mafuriko mara kwa mara, ni wakati mwafaka kwao kuhama au kuchukua hatua zinazotakiwa katika kujihadhari.

Kadhalika, wakati wa mvua kubwa kama hizo, kumekuwa na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu, kuhara na kuhara damu ambayo chanzo kikuu ni uchafu. Kwa mantiki hiyo, tahadhari pia zinapaswa kuchukuliwa katika kudhibiti magonjwa hayo ambayo yamekuwa yakigharimu maisha ya watu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Magonjwa yasiyo ya kuambukiza yaja kwa kasi, sote tujiulize tahadhari tunazochukua

Na Sabato Kasika

**ZAIDI** ya asilimia 70 ya vifo vinavyotokea nchini na duniani kote, husababishwa na magonjwa ambayo si ya kuambukiza ambayo ni kisukari, shinikizo la juu la damu na kifua sugu.

Katika msururu huo wa magonjwa yasiyoambukiza, mengine ni pumu na uzito uliopindukia, ambayo pia inaelezwa kuwa yanazidi kuongezeka kuliko magonjwa yanayoambukiza.

Ugonjwa wa shinikizo la juu la damu unatajwa kuongezeka zaidi nchini, kutokana na mtindo wa maisha, ikiwamo ulaji usiyofaa, matumizi ya chumvi, msongo wa mawazo, matumizi ya wanga kwa wingi kuliko mboga na matumizi ya mafuta kwa wingi na kutokufanya mazoezi.

Hayo ni kwa mujibu wa Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dk. Mwanaada Kilima, anayegusia ugonjwa wa kisukari na kufafanua kipo cha aina mbili.

Katika ufafanuzi wake, ni kwamba kuna kundi la wanaopata kisukari kisichozuilika na kuna kundi ambalo wanapata kisukari ambacho kinazuilika na kwamba asilimia kubwa ya ugonjwa wa kisukari huchangiwa na mtindo mbaya wa maisha.

Kwa kuwa inaonekana chanzo cha kuwapo kwa magonjwa hayo ni mtindo wa maisha, ninadhani ipo haja kwa kila mmoja wetu kujijengea tabia ya kula mlo kamili na kufanya mazoezi ili kuepuka magonjwa.

Pia kuna suala la kupunguza matumizi yaliyokithiri ya chumvi, sukari na mafuta ya kupikia kwa kuzingatia ushauri wa muhimu unaotolewa na madaktari.

Njia hiyo inaweza kutusaidia kuwa nje ya asilimia 70 ya vifo vinavyotokea nchini na duniani kote, kwani ni uamuzi tu wa kila mmoja kulinda afya yake kwa kubadili mtindo wa maisha.

Mwezi ujao kuanzia tarehe 5 hadi 12, kutakuwapo Wiki ya Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, hivyo ninadhani ni wajibu wa kila mmoja kulinda afya yake dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

**Takwimu hizo zinaendelea kuweka wazi jinsi ambavyo ni muhimu Watanzania kuangalia kila iwezekanavyo kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya kwa lengo la kuepuka magonjwa hayo.**

Ikumbukwe, katika maadhimisho ya mwaka jana, ilielezwa kuwa magonjwa yasiyoambukiza ni miongoni mwa sababu za ongezeko la vifo nchini na kwamba kila vifo 100, vifo 33 vinatokana na magonjwa ya kundi hilo.

Takwimu hizo zinaendelea kuweka wazi jinsi ambavyo ni muhimu Watanzania kuangalia kila iwezekanavyo kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya kwa lengo la kuepuka magonjwa hayo.

Vilevile inaelezwa kuwa magonjwa hayo yameongezeka mara tano hadi tisa zaidi kati ya miaka ya 80 ambapo asilimia moja tu ya Watanzania walikuwa na tatizo la kisukari na asilimia tano walikuwa na tatizo la shinikizo la juu la damu.

Inaelezwa kwamba, kwa sasa tatizo la kisukari limeongezeka na kufikia asilimia tisa wakati tatizo la shinikizo la juu la damu limeongezeka zaidi na kufikia asilimia 25. Hizo ni takwimu za Wizara ya Afya, zinazoonyesha ongezeko kubwa la magonjwa hayo katika kipindi cha Julai 2022 hadi mwaka huu.

Inaelezwa kuwa magonjwa yasiyoambukiza ambayo yalisababisha wagonjwa wengi kuhudhuria vituo vya huduma za afya ni shinikizo la juu la damu wagonjwa 1,456,881 sawa na asilimia 49 ukilinganisha na asilimia 34 kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

Kisukari kinatajwa kuwa na wagonjwa 713,057 sawa na asilimia 24, magonjwa ya mfumo wa hewa ni wagonjwa 386,018 sawa na asilimia 13 ikilinganishwa na asilimia 10 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

Kuishi bila kuwa na magonjwa yasiyoambukiza inawezekana, iwapo kila mmoja atachukua tahadhari kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ambayo yanaelekeza kubadili mtindo wa maisha.

## Wadaiwa kutumia jina la Ofisa Madini kutapeli wachimbaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

OFISA Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Jeremiah Hango, amesema kumeibuka kikundi cha watu wanaotumia jina la ofisi yake kikizunguka katika maeneo yenye shughuli ya uchimbaji madini na kuwatapeli wachimbaji.

Ni hali aliyoitaja kuzua migogoro isiyoisha katika maeneo ya wachimbaji hususani wachimbaji wadogo kutokana na watu hao kukusanya fedha kwa wachimbaji kinyume cha sheria.

Hango alibainisha hayo jana ofisini kwake alipozungumza na waandishi wa habari wilayani hapa na kueleza kuwa ofisi yake kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama inashughulikia tatizo hilo kwa kuwatafuta matapeli hao.

Alisema kuwa watu hao wakibainika watachukuliwa hatua za kisheria ili kukabiliana na migogoro isiyokuwa na tija kwenye maeneo yenye uchimbaji hususani kwa wamiliki wa mashamba na wenye leseni za uchimbaji.

Aliwataka wachimbaji wadogo wa madini kutambua kuwa katika sekta ya madini kuna wizara mbili ambazo zinahusika na utatuzi wa migogoro mbalimbali inayoibuka kwenye maeneo ya wachimbaji; Wizara ya Madini na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Na kila Wizara ina majukumu yake ya kiutendaji.

Alifafanua kuwa kama mgogoro unahusu ardhi, wao hawatahusika nao kwa kuwa jukumu lao ni kusimamia wachimbaji wachimbe kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

Ofisa Madini huyo aliwataka wachimbaji kuacha kulalamika na kuwanyooshea vidole na badala yake wafike katika mabaraza ya kata na kupata suluhu.

Alisema katika mgodi mdogo Mwime ulioko Kata ya Zongomela, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, kuna mgogoro baina ya mmiliki wa shamba lenye madini na mmiliki wa leseni ya uchimbaji na unatakiwa kutatuliwa na Baraza la Ardhi la Wilaya na si vinginevyo.

Alisema wachimbaji wadogo wanatakiwa kuendelea na shughuli zao za uchimbaji wa madini wakati mgogoro huo ukitatuliwa na baraza, mmiliki wa leseni hatoruhusiwa kuchukua mapato yoyote hususani mifuko yenye mawe yanayosaidikiwa kuwa na madini na yatatunzwa na serikali mpaka hapo mgogoro huo utakapotatuliwa.

Pia alisema ofisi ya madini ilimwelekeza mmiliki wa leseni, Kembo and Partners kuwasilisha nyaraka zinazohusu shamba hilo kwa mujibu wa matakwa ya barua aliyoandikiwa yenye kumbukumbu Na.HA.366/457/278/08 ya tarehe 03/10/2023 kama Sheria ya Madini kifungu Na.95 (a) (1) ya Sheria ya Madini Sura Na.123 inavyotaka na si vinginevyo.




Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, SSP Solomon Mwangamilo (kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya Mobile App, itakayowezesha askari wa kikosi hicho, kukusanya taarifa za ajali zinazotokea barabarani yaliyowezeshwa na kampuni tanzu ya TBL na AB InBev. Wengine ni Mkurugenzi wa Usambazaji TBL, Nancy Riwa (wa tatu kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EALA yapitisha azimio kumpongeza Dk. Tulia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BUNGE la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), limepitisha azimio la kumpongeza Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Akiwasilisha katika mkutano wa Bunge hilo ulioanza jana jijini Arusha, hoja ya kuliomba Bunge lipitishe azimio la kumpongeza Dk.Tulia, Mbunge Dk. Shogo Sedoyeka (Tanzania), alisema uwakilishi wa Dk.Tulia, siyo kwa Tanzania pekee, bali ni alama ya uwezo wa uongozi kwa wanawake wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Afrika kwa ujumla.

"Wanawake wanaweza na huu ushindi wa Dk.Tulia ni jibu tosha kwa nchi za Afrika na EAC, kuwa wanawake wanaweza kuongoza nafasi mbalimbali ngazi za juu, ikiwamo vijana kutumia fursa za kugombea nafasi mbalimbali bila kuogopa na kuondoa hofu," alisema.



Alisema uchaguzi huo umedhihirisha uwezo wa Afrika, kujiamulia mambo yake.

James Ole Milya, Mashaka Ngole (Tanzania) na David Ole Sankok (Kenya), walisema umoja ulioonyeshwa na nchi za (EAC), wakati wa kampeni ya kuwania kiti cha Rais wa IPU, ni kielelezo na mfano wa kuigwa katika mambo mengine yenye maslahi kwa jumuiya hiyo.

"Kwa hili la ushindi wa Spika Tulia, ni dhahiri kuwa nchi za EAC, ziliweka nyuma tofauti zake na kumunga mkono kwenye kampeni yake na kisha ushindi huu tumeupata.

Huu ni ushindi wa wanajumuiya, wote tunashukuru sasa abebe majukumu mbalimbali ikiwamo utatuzi wa changamoto zitakazotokea, lazima dunia na nchi za Afrika zijuwe, wanawake wana uwezo mkubwa katika maamuzi mbalimbali," alisema Sankok.

Mbunge, James Ole Milya (Tanzania), alisema ushindi wa Spika Tulia umeonyesha nguvu ya ukomavu wa kisiasa kwa wanawake, vijana na jamii mbalimbali, katika kuhakikisha maendeleo yanakua kwa kasi katika nchi za Afrika.

Akiwa Rais wa 31 wa IPU, Dk.Tulia pia ameweka rekodi ya kushikilia kiti hicho akiwa mwanamke wa kwanza, kutoka Afrika na ataongoza umoja huo kwa kipindi cha miaka mitatu, nafasi hiyo pia iliwahi kushikiliwa na Najma Heptulla kutoka India mwaka 1999.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# Jela maisha kwa kunajisi wajukuu

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa imemhukumu kifungo cha maisha gerezani Joseph Nyansio (40), mkazi wa Kijiji cha Kasekela wilayani Sumbawanga baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kunajisi wajukuu wake wawili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Shadrack Masija, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, alisema watoto hao (majina yamehifadhiwa) wana umri wa miaka minane na saba.

Alisema kuwa mchana wa Juni 29 mwaka huu, mtuhumiwa huyo alidaiwa kuwalaghai watoto hao kuwa anawapeleka shambani ili akawachumie matunda ndipo alipowafanyia kitendo hicho.

Kamanda huyo alisema kuwa baada ya mtuhumiwa kukamatwa na upelelezi kufanyika, alifikishwa mahakamani mbele ya Hakimu Thomas Bigambo na baada ya ushahidi kukamilika, Oktoba 30 mwaka huu alihukumiwa kifungo cha maisha gerezani.

Kamanda Masija alitoa wito kwa wanaume mkoani mwake kuacha kuendekeza tamaa za kimwili, akizitaja zimekuwa sababu za kuwafanyia matukio ya kikatili watoto na ndugu zao na kuishia kuhukumiwa vifungo gerezani.

Pia aliwataka wananchi kuacha imani potofu za kishirikina kwa kuwa nazo zimekuwa chanzo kikubwa cha maovu mkoani mwake.

Aliwataka wajikite katika kufanya kazi za maendeleo ili kupata mafanikio halali katika maisha yao.



Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Upasuaji wa Fistula kutoka Hospitali ya CCBRT, Peter Majinge (mwenye miwani), akiongoza jopo la wataalamu wa afya kutoka hospitali hiyo na ya Mkoa wa Lindi, kutoa matibabu kwa mmoja wa wanawake wenye tatizo la fistula katika kambi ya matibabu ya ugonjwa huo inayoendelea mkoani humo jana. Tangu mwaka 2019 CCBRT, Equinor Tanzania na Mkoa wa Lindi, wamekuwa katika ubia wa kutoa matibabu ya fistula kwa wanawake mkoani humo, sambamba na kuwawezesha kiuchumi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi majitaka kuwanufaisha 11,480

**Na Joseph Mwendapole**

MRADI wa kuondoa majitaka wa Mbezi Beach, Kinondoni, Dar es Salaam unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 124, utawanufaisha wananchi 11,480.

Ni mradi unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA). Unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18.

Jana jijini Dar es Salaam, Mhandisi wa Mradi, John Romanus, alibainisha hayo katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata ya Kawe. Alifuatana na Diwani wao, Muta Rwakatare.

Mkutano huo uliratibiwa na uongozi wa Kata ya Kawe kwa lengo la kujadili utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata hiyo.

Romanus alisema mamlaka imeanza utekelezaji wa mradi huo na kazi inaendelea vizuri. Wanapata ushirikiano wa wananchi na uongozi wa kata.

Alisema DAWASA itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa mradi huo na namna unavyotekelezwa katika maeneo yao ili kila mmoja atoe mchango wake.

"Tayari mkutano mkubwa wa kuutambulisha kwa ngazi ya kata umefanyika, ukihusisha ofisi ya Mkuu wa Wilaya na tutaendelea kuelimisha wananchi kuhusu mradi huu," alisema.

Romanus alisema kwa sasa utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 15 na kazi ya kulaza mabomba inaendelea katika maeneo yaliyoainishwa kwenye usanifu wa mradi.

Alisema mradi huo unalenga kuboresha usafi wa mazingira katika kata nne za Dar es Salaam; Mbezi Beach, Kunduchi, Salasala na Kawe ili kuepusha hatari ya magonjwa ya mlipuko.

Katika mkutano huo, Diwani Muta alitaka DAWASA iongeze kasi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa utekelezaji mradi huo mkubwa wa uondoshaji majitaka.

Alisema wananchi wakielimishwa kuhusu mradi huo wa kuondoa majitaka majumbani, watashiriki na kusaidia katika kuboresha usafi wa mazingira kwenye maeneo hayo.

Alisema mradi wa kuondoa majitaka Mbezi Beach ni muhimu na wananchi wengi wameonesha kuufurahia kwa sababu unalenga kuondoa changamoto inayosumbua eneo hilo kwa muda mrefu.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa na kawaida ya kutiririsha majitaka kwenye barabara za mitaa na kusababisha hatari ya magonjwa ya mlipuko. Diwani huyo alisema serikali kupitia DAWASA imewekeza fedha nyingi katika kutekeleza mradi huo na matarajio ya wananchi ni kuona kero hiyo iliyodumu kwa muda mrefu inafika ukomo.

"Hivyo, niwatake DAWASA kuongeza bidii ya kuwaelimisha wananchi wajue nia njema ya serikali kwao, manufaa ya mradi huu, utapita maeneo gani na mradi utakamilika lini ili na wao washiriki vyema katika kulinda miundombinu itakayowekwa kwenye mradi huu.

"Niwapongeze DAWASA kwa kazi nzuri mnayofanya ya kutekeleza mradi huu na nimeona kazi inaendelea kwenye mitaa mbalimbali, hivyo niwakumbushe kulisimamia hili ili tija ya kazi hii ionekane kwa wanufaika," alisisitiza Rwakatare.

Alisema ana uhakika elimu ikitolewa kwa wingi na wananchi wakaelewa, wataacha tabia ya kutupa taka ngumu kwenye miundombinu ya kuondoa majitaka na kutunza miundombinu hiyo.

Aliwataka viongozi wote wa kata kushirikiana vyema na DAWASA kwa kuwaonesha maeneo na mitaa yote yenye changamoto ili wajue namna ya kupitisha mabomba na kurahisisha utekelezaji kazi hiyo.

## Mbunge azipatia vifaa sekta za afya na elimu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini (CCM), AbdulAziz Abood, ametoa vifaa tiba kwenye zahanati na vituo vya afya 10.

Vilevile, ametoa seti za kompyuta na mashine za kudurufu kwa shule za kata hizo zilizoko Manispaa ya Morogoro vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 105, akitamba yeye ni mbunge wa vitendo zaidi na siyo wa majukwaani.

Ametoa msaada huo ni siku chache baada kukabidhi magari matatu ya kubeba wagonjwa katika kata za Lukobe na Tungi na Hospitali ya Manispaa ya Morogoro, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200.

Akizungumza na wananchi kwa nyakati tofauti wakati wa kukabidhi misaada hiyo katika kata 10, Abood alisema katika sekta ya afya vifaa tiba hivyo vimegharimu Sh, milioni 80 wakati vifaa katika sekta ya elimu vimegharimu Sh. milioni 25.

"Mimi nipo kama Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, hana muda wa kujibishana na wapinzani majukwaani, yeye anafanya kazi kwa vitendo tu na wote tunaona kazi kubwa anayofanya.

"Na mimi nipo hivyo hivyo, sina muda wa kupanda majukwaani kuwajibu wapinzani, hapa ni vitendo tu na wote mnanifamu," alitamba.

Abood alivitaka vifaa tiba hivyo ni pamoja na darubini, kifaa cha kutenganisha selamu na seli za damu, kifaa cha kupima sukari mwilini, vitanda vya wagonjwa, mitungi ya gesi na vifaa vingine vya maabara vya kupimia magonjwa mbalimbali.

Kwa upande wa sekta ya elimu, Mbunge Abood alitoa seti za kompyuta kwa shule za msingi na sekondari, madawati, mashine za kudurufu pamoja na kuchangia ujenzi wa majengo mbalimbali vikiwamo vyoo kwa shule zenye upungufu wa matundu ya vyoo.

Alisema ameamua kutoa misaada hiyo baada ya kufanya ziara zake katika kata zote 30 za Manispaa ya Morogoro na kubaini kila moja ina changamoto zake katika sekta hizo.

Mbunge Abood alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kusaidia sekta hizo kupata huduma bora za kiafya na elimu.



# Nyalandu aibukia Samia Love

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

ALIYEWAHI kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Mbunge wa Singida Kaskazini, Lazaro Nyalandu, ameibukia katika safari ya matumaini ya 'Samia Love' inayolenga kutoa msaada wa uchunguzi wa kibingwa wa magonjwa na matibabu yake, ikiwamo huduma ya upasuaji.

Nyalandu ambaye kwa sasa ndiye Mratibu wa Kampeni ya Samia Love, alikutana jana na wagonjwa waliopona katika Hospitali ya Misheni ya Seliani LMC inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Wagonjwa 400 kutoka maeneo mbalimbali walifanyiwa upasuaji na timu ya madaktari bingwa 60 wa mifupa na nyonga kutoka Los Angeles, Marekani.

Akiwa na mashuhuda hao waliopona, Nyalandu alidokeza ujio mwingine wa madaktari hao kutoka Marekani, wanaotarajiwa kutua nchini kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma ya afya.

"Wengi wamekuwa wanatamani kuja kutoa huduma hii baada ya jopo la kwanza kurudi na kusimulia kile kilichofanyika nchini. Niahidi kwamba kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais wetu, Samia Suluhu Hassan, tunatarajia kuleta madaktari wengine," alisema Nyalandu.

Mwezi Agosti mwaka huu, timu ya madaktari hao iliyoalikwa na Rais Samia iliyokuwa inaongozwa na kaulimbiu 'Upendo wa Mama, Rais Samia Suluhu Hassan kwa wananchi wake', iliwaona wagonjwa 400 waliokwenda katika hospital hiyo.

Baadhi ya mashuhuda waliopona akiwamo Faidha Mtwana aliyefanyiwa upasuaji wa nyonga, walishukuru kwa matibabu hayo.

Faidha alisema kuwa kwa sasa anafanya kila kitu na anapata usingizi mzuri kwa kuwa hapo awali alikuwa hawezi kulala kutokana na maumivu makali.

# NCAA yapewa mabilioni kutekeleza mradi Jiopaki

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

**Utiaji saini mkataba huo unaotarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2024, ulifanywa jana na NCAA na ujumbe maalum wa Serikali ya China.**

SERIKALI ya China imeipa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) Dola za Marekani milioni 9.5 (Sh. bilioni 25) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa uboreshaji na uendelezaji wa Jiopaki ya Ngorongoro/Lengai.

Jiopaki ya Ngorongoro/Lengai, ni Jiopaki pekee iliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, inayotambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Katika hafla ya utiaji saini mkataba wa makubaliano ya awali ya utekelezaji mradi huo uliopewa jina la Ngorongoro/Lengai Unesco Global Geopark, Kamishna wa Uhifadhi NCAA, Richard Kiiza, alisema msaada huo wa fedha ni matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya China Novemba 20, 2022.

Utiaji saini mkataba huo unaotarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2024, ulifanywa jana na NCAA na ujumbe maalum wa Serikali ya China. Ni mradi wa miaka miwili.

"Unajua China wanapendelea zaidi utalii wa miamba badala ya wanyama. Kwahiyo, tunatarajia kwamba baada ya kupata msaada huu na kuendeleza maeneo tuliyoyalenga, tunategemea kupata wageni wengi kutoka China.

"Manufaa ya moja kwa moja ya msaada huu ni kuboresha miundombinu ya utalii, kuboresha barabara, kujenga vyoo, kujenga makumbusho ya kijiolojia, kujenga sehemu za wageni kupumzika na kuona vivutio mbalimbali vilivyoko katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro," alisema.

Kabla ya utiaji saini makubaliano hayo, Meneja Urithi wa Utamaduni na Jiolojia wa NCAA, Joshua Mwankunda, alisema Jiopaki hiyo ya Ngorongoro/Lengai, inachukua maeneo ya Ngorongoro kwa asilimia 90 na Wilaya zinazopakana na Ngorongoro.

Kwa mujibu wa Mwankunda, kupitia msaada huo wa serikali ya China kwa Tanzania, NCAA inakwenda kuendeleza Jiopaki ya Ngorongoro/Lengai, ambayo itaacha alama katika sekta ya utalii.



Wadau wa madini ya Tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wakifuatilia mdahalo wa ushiriki imara wa wanawake katika shughuli za madini ulioandaliwa na Shirika la Civil Social Protection Foundation (CSP), juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kilichojificha viongozi wa dini kuchelewa kukemea ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MCHUNGAJI Kiongozi wa Usharika wa Lole wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Zablon Mtui, amesema viongozi wengi wa dini wanachelewa kukemea matukio ya ukatili wa kijinsia kwa kuwa jamii inadhani kuwaficha taarifa za ubakaji, ulawiti na vipigo kwa wanawake na watoto ni ustaarabu.

Amesema bado vita hiyo ya ukatili wa kijinsia, inakabiliwa na tatizo la msingi la jamii kuwaona wanaharakati au wanaopaza sauti kufichua hali hiyo ni wadhalilishaji.

Mch. Mtui alikuwa anatoa nasaha zake jana kwa wananchi wa Kijiji cha Lole, Kata ya Mwika Kaskazini, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro wakati wa mkutano wa utoaji elimu kwa umma.

Mkutano huo uliendeshwa na shirika la kiraia la KWIECO linalofadhiliwa wa Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust) kupitia mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya wanawake na watoto.

"Ifike mahali wote tuone tuna kazi kubwa ya kufanya ya kupaza sauti kuhusu ukatili wa kijinsia. Kama mchungaji, nimekuwa ninajiuliza mbona kuna vitu vinatajwa kwenye jamii yangu hiihii lakini sivijui?

"Ni kwa sababu jamii yetu inafanya ustaarabu wa kunyamazia baadhi ya mambo, halafu akitokea mtu anapaza sauti wanasema anatudhalilisha. Si kwamba amewadhalilisha, ile sauti yake inasaidia.

"Mimi ninaamini mambo mawili yakifanyika, yatasaidia kupunguza ukatili. Huko kwenye jamii kila mtu anatakiwa akae kwenye nafasi yake na asaidiwe kukaa kwenye nafasi yake. Baba hawezi kuwa mama na mama hawezi kuwa baba," alisema.

Kutokana na kushamiri kwa matukio hayo, Mch. Mtui, alionya jamii kuacha kupoka majukumu yasiyo yao.

"Pale baba anapokwama kukaa kwenye nafasi yake, mama hapaswi kufurahia, kwa sababu mume ameshindwa na yeye akafikiri anaweza kuwa baba, hilo haliwezekani!" alisisitiza.

Akitoa elimu kwa wakazi wa kijiji hicho, mratibu wa mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya wanawake na watoto, Veronica Ollomi, aliwasihi wananchi hao kuchukua hatua.

"Hebu tuchukue hatua, kama baba una wajibu gani katika familia, tusiachie kinamama peke yao uangalizi wa watoto. Biblia inasema mtoto akiharibika, mwana mpumbavu ni mzigo kwa mamaye. Tutimize wajibu wetu, wewe kama baba wa familia umekaaje kwenye nafasi yako?

"Mchungaji anaweza akahubiri kanisani, akatumia na Biblia, lakini hafiki kila mahali, ninyi mkiwa kanisani, ataongea na ninyi, lakini kwenye ngazi ya kaya kule hajui, labda mtu aende akamwambie.

"Tunazo kesi nyingi za watoto wa kiume kulawitiwa, jamani mchungaji! Kama ni kufunga tufunge kwa sala ili kuwanusuru watoto wa kiume.

"Kesi za watoto kulawitiwa na kubakwa zimekuwa tishio na si kwamba ni vitu vya kuficha, lakini ni kwa vile tu jamii tumeamua kuvifumbia macho, kukaa na kuendelea na maisha yetu," alisisitiza mratibu huyo.



# Viongozi 19 wa vijiji mbaroni tuhuma mauaji

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

ZAIDI ya watu 19 wakiwamo wa jeshi la jadi 'Sungusungu', Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, wanashikiliwa na polisi mkoani hapa kwa tuhuma za mauaji ya vijana wawili waliodhaniwa kuwa ni wezi.

Vijana hao Nkula Lameck (26), mkazi wa Mwamanga na Nzuri Kazungu (25), mkazi wa Ichobela wilayani Magu, wanadaiwa kuuawa Oktoba 31, katika kijiji na Kata ya Mwaniko na watu wanaodaiwa kuwa na hasira kali wakiwatuhumu kuiba gunia la mpunga na kuku.

**Naagiza chukua viongozi hawa wote waende wasaidie jeshi la polisi hawezekani mpaka sasa hivi eti tuna viongozi hapa na tukio limetendeka mpaka sasa hakuna lolote walililolifanya juu ya tukio.**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alitoa taarifa ya kukamatwa kwa watu hao jana wakati akizungumza na wananchi kijijini hapo na kuwaonya kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi.

Vilevile, alimuagiza Mkuu wa Polisi wilayani humo kwa kushirikiana na Mkuu wa Polisi wilayani Kwimba kumtafuta na kumkamata mtu anayedaiwa kuibiwa mali hizo kwa kuwa anaweza kuhusika katika tukio hilo kwa kutoa taarifa za kukamatwa kwa vijana hao.

Alisema vijana hao walioku-wa wamebebana katika pikipiki yenye namba za usajili MC 989 CWU, majira ya saa 11.30 jioni wakitokea Budulu-Ngudu Kwimba, walishambuliwa kwa silaha za jadi pamoja na mawe hadi kufa huku pikipiki yao ikichomwa moto na kuteketea.

"Jeshi la polisi hatuwezi kukaa kimya pasipo kuchukua hatua wakati kuna mambo ya ovyo yaliyotendeka na kama watu hawa wangekuwa na makossa kiasi gani zipo sheria za kuchukua ikiwa ni kuwakamata na kuwafikisha polisi ambapo mahakama pekee ndiyo inayotoa hukumu baada ya uchunguzi."

Alisema, jeshi hilo litawafikisha mahakamani viongozi wote wa eneo hilo ambao walikuwa wazembe katika tukio hilo baada ya kukamatwa na kuhojiwa hadi kuamua kuwahukumu wao wenyewe.

"Naagiza chukua viongozi hawa wote waende wasaidie jeshi la polisi hawezekani mpaka sasa hivi eti tuna viongozi hapa na tukio limetendeka mpaka sasa hakuna lolote walililolifanya juu ya tukio," aliagiza SACP Mutafungwa.

Alisema jeshi hilo lilifuatilia na kubaini kuwa vijana hao hawakuwa na makosa kwa kuwa hata vitu hivyo walivyokuwa wanadai kuwa vimeibiwa hawakukutwa navyo.

"Watu wamejitetea na kuwaambia kuwa wanatoka kutoa mahari, lakini nyie mkaamua kuwaua kama kuku hatuwezi kuvumilia vitendo vya namna hii lazima wote waliosababisha vifo hivi watawajibika ipasavyo," alieleza SACP Mutafungwa.

Alimuagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Misungwi kuendelea kubaki katika eneo hilo na kuhakikisha anapata taarifa za watu wote waliohusika na mauaji hayo na kuhakikisha wanakamatwa ili sheria ichukue mkondo wake.

Kadhalika, alisema jeshi hilo limekuwa likitoa elimu kupitia askari kata waliopo katika maeneo husika, lakini anaona bado watu wameendeleza vitendo vya kujichukulia sheria mkononi na kuahidi kuwashughulikia wote wanaokiuka taratibu za kisheria makusudi.



Mwenyekiti cha Kijiji cha Mwaniko Ezron Ntonja (katikati mwenye kofia), Mtendaji wa Kijiji hicho, Heleni Severine pamoja na Kiongozi wa jeshi la jadi 'sungusungu' (kushoto), wakiwa kwenye gari la polisi, baada ya kukamatwa kufuatia agizo la Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza SACP Wilbroad Mutafungwa (hayupo pichani), baada ya kutokea tukio la wananchi kujichukulia sheria mkononi na kuwaua vijana wawili wakiwatuhumu kuwa wezi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Kesi sita za mauaji kurindima Mahakama Kuu

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Shinyanga imeanza kusikiliza mashauri ya kesi sita za mauaji zinazowakabili washtakiwa mbalimbali wanaodaiwa kutekeleza matukio hayo katika maeneo tofauti wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Mashauri hayo yanasikilizwa chini ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama kuu Kanda ya Shinyanga, Frank Mahimbali, baada ya upelelezi wa mashtaka hayo kukamilika na mahakama hiyo imeanza kusikiliza mashahidi katika kesi hizo.

Hayo yalibainishwa juzi na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Edmund Kente, wakati akizungumza na vyombo vya habarai wilayani hapa na kueleza kuwa kesi hizo zitasikilizwa mfululizo mpaka zitakapotolewa hukumu.

Kente alisema kuwa katika mashauri hayo washtakiwa walidaiwa kutenda makosa hayo kuanzia mwaka 2021 ikiwa kwa sasa shauri moja limeanza kusikilizwa siku moja iliyopita na linatarajiwa kuwa na mashahidi wanane.

Alisema katika shtaka hilo ambalo hakutaja wahusika, mashahidi sita wamesikilizwa na juzi walikuwa wakisikilizwa mashahidi wengine wawili mpaka kesi kufikia hatua ya kuzitolea hukumu.

"Mashauri ya mauaji kwa sasa takwimu zake zimeenda zikipungua, lakini ninatoa wito kwa wananchi wakiona kuna viashiria vyovyote vya vitisho vinavyoweza kusababisha mauaji watoe taarifa kwenye vyombo vya dola na badaye kuja kuisaidia mahakama katika ushahidi," alisema Kente.

Alisema kesi za mauaji ziko tofauti kwa kuwa kisheria hazina dhamana na pia zina ukomo wa muda wa upelelezi na unachukua muda mrefu kutokana na ofisi ya Mkemia wa Serikali kuzidiwa.

Aidha, aliwataka wananchi kuwa tayari kutoa ushahidi wa kweli baada ya kubaini wapo wanaopangwa bila kushuhudia tukio husika na kuisababishia usumbufu mahakama.

# Anayedaiwa kutumia bangi asota mahabusu

**Na Remmy Moka,** SAUT

SALMA Abdallah (37), mkazi wa Lumala, wilayani Ilemela mkoani Mwanza, anayekabiliwa na shtaka la kujihusisha na matumizi ya bangi ameendelea kusota mahabusu baada ya kukosa dhamana.

Salma alifikishwa mahakamani hapo juzi akikabiliwa na kesi ya jinai.

Akimsomea shtaka hilo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Amani Sumari, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Monika Mweli, alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo kati ya Oktoba mosi, mwaka huu katika eneo la Lumala, wilayani Ilemela.

Mshatakiwa huyo alikana kutenda kosa hilo na Hakimu alipanga tena shauri hilo hadi Novemba 13, 2023 litakapoitwa kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali ya shtaka linalomkabili.

Aidha, Salma alirejeshwa rumande kutokana na kutokidhi masharti ya dhamana baada ya kutakiwa kuwa na wadhamini wawili na kila mmoja kusaini bondi ya maneno ya Shilingi milioni mbili kila mmoja, kitambulisho pamoja na barua ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa.

**Mshatakiwa huyo alikana kutenda kosa hilo na Hakimu alipanga tena shauri hilo hadi Novemba 13, 2023 litakapoitwa kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali ya shtaka linalomkabili.**



Ukurasa 12

## Mratibu Chanjo: Kuna kundi kubwa nchini halijamaliza dozi Uviko-19



## MAJIBU YA MMAM KITAIFA... Rais Samia:Vifo vya uzazi vimepungua 80%, kusuasua wenye chini ya miaka 5

Ukurasa 14

ITIKADI KUPOKEZANA KIJITI…

# Samia anaijengea wilaya hospitali hadhi ya mkoa na zawadi zahanati, vituo afya

## •Zaambatana na 'ambulance' za maboti...

**Na Neema Emmanuel, UKEREWE.**

WILAYA ya Ukerewe sasa katika Tanzania Awamu ya Sita, inajinasibu na nuru ya maendeleo kiafya, huku wenyeji wanapogeuza uso nyuma, wanakiri wametoka mbali kupambana kupata huduma bora za tiba.

Ni simulizi yenye mzizi katika uongozi wa Rais Dk. John Magufuli, wakazi wakimpa kilio kutaka huduma bora za afya, pale alipozuru wilayani Ukerewe mwaka 2018; zama Samia Suluhu Hassan, wakatk huo alikuwa Makamu wa Rais.

Ilikuwa papo kwa hapo, Rais Dk. Magufuli, akaagiza kutekelezwa ombi lao chini ya wizara mama inayohusika na afya. Baada ya kifo chake, Rais Dk. Samia mwaka 2021, akaendeleza dhamira katika utamaduni wa kupokezana viti vya uongozi, ahadi wakati huo ilikuwa haijatekekezwa

Hapo, Rais Dk, Samia akaendeleza ahadi kwa kauli na vitendo, akiongeza mengine ya afya za msingi; zahanati na vituo afya, kama alivyoahidi akichukua uongozi wa nchi, Machi, 2021.

Sura ya utekelezaji baada ya agizo la Rais Dk. Magufuli, ikashuhudiwa mara ya kwanza kupitia mkazo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Septemba, 2020 zama za Awamu ya Tano na akarejea tena Oktoba mwaka jana katika zama Awamu ya Sita, akiuhakikisha rasmi umma Ukerewe kuhusu utekelezaji wa Rais Dk. Samia, mradi umo katika bajeti ya mwaka.



Kituo cha afya kipya wilayani Ukerewe. **PICHA ZOTE: RESTUTA JOSEPH.**

Kutimu Novemba 25 mwaka jana, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango akawa wilayani Ukerewe, alikowahakikishia tena kuiva hatua za ujenzi wa hospitali, akibeba salamu za Rais Dk. Samia, iwe na hadhi ya mkoa- rufani, kuwakomboa wana - Ukerewe wasitaabike kufuata huduma jijini Mwanza, vigezio na masharti kuvuka maji ya Ziwa.

Pia, Dk. Mpango akaiagiza Wizara ya Afya inayosimamia mradi kufika Ukerewe kushughulikia suala hilo. Hadi Desemba mwaka jana, Waziri wa Afya, alishafika Ukerewe kwa maandalizi ya awali.

Kimsingi, hatua iliyochukuliwa na Halmashauri ya Wilaya Ukerewe hadi sasa, imeshatenga ekari 16 katika kijiji cha Bukindo kata ya Bulamba.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, Juni mwaka huu akiwa Ukerewe baada ya kukagua ekari hizo 16, akatoa ufafanuzi patakavyojengwa hospitali yenye hadhi ya rufani mkoa.

"Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe ambayo ilitarajiwa kuwa ya mkoa, kwa sasa itaendelea kuwa hospitali ya wilaya, hospitali ya rufani ya mkoa itajengwa katika kata ya Bulamba, kijiji hiki cha Bukindo," akafafanua Waziri Ummy.

Pia, waziri anakiri kwa kushirikiana na wataalamu wake, wameridhishwa na eneo hilo, mradi ulipokuwa katika hatua ya uchoraji ramani, kuwezesha kujua thamani ya kujenga hospitali ikijikita kuhudumia; upasuaji, magonjwa ya wanawake na uzazi, pia tiba za watoto, ukitarajiwa kuwa na watumishi zaidi ya 50.

"Tutoe ushirikiano kwa watumishi wa afya wakituambia tujenge vyoo bora tujenge ili tuweze kujikinga na magonjwa ya milipuko kama kipindupindu, pia tuwapeleke watoto kupata chanjo," anatamka Waziri Ummy.

Waziri Ummy anaendelea: "Baada ya Mheshimiwa Rais (Dk. Samia) kusikia kilio cha wana-Ukerewe, amefanya maamuzi bora ya kuwaletea hospitali hii ambayo itakuwa ni ghorofa mbili, hii haijawahi kutokea. Ni kwa sababu ya mapenzi yake kwenu."

Mganga Mkuu wa Wilaya Ukerewe, Dk. Charles Mkombe, anaithibitishia Nipashe wiki hii, pesa za ujenzi zimeshapatikana shilingi bilioni tano, hatua inayoendelea sasa ni tenda ya kumpata mjenzi.

Dk. Mlowe anafafanua kwamba, hospitali itakuwa na hadhi sawa na Sekou Toure ya jijini Mwanza, huku Bugando ikibaki ngazi ya Kanda.

**PICHA INAYOTAWALA**

Ni simulizi ngumu kwa wanawake walienda hospitali na maji ya mtoni au kutoka nayo nyumbani, pindi wanapofuata huduma za afya, katika Hospitali ya Wilaya Ukerewe.

Leo ndani ya zama Awamu ya Sita, historia imebadilika kwa safari kilomita 15 kubeba maji kufuata huduma ya upasuaji na mengineyo, sasa kila kitu kiko hospitalini.

Hapo ni baada ya Halmashauri ya Wilaya Ukerewe, katika mwaka wa fedha, 2022/23 ulioisha Juni mwaka huu, iliyosimamia uwekezaji zaidi ya shilingi billioni tano kwa miradi ya afya, ikiwamo ukarabati wa zahanati na vituo vya afya.

Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Igalla, Dk. Jeremiah Katwale, anaieleza Nipashe kwamba kituo hicho kinahudumia zaidi ya wakazi 17,412 kutoka vijiji vitano na mpaka sasa ujenzi umefika asilimia 98, kwa matarajio ndani ya muda

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Mratibu Chanjo: Kuna kundi kubwa nchini halijamaliza dozi Uviko-19

**Na Beatrice Moses**



Hali ilivyokuwa kwenye uzinduzi wa chanjo ya Uviko-19 nchini, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ni sehemu ya washiriki. **PICHA: MTANDAO**

KWA sasa inatajwa, baadhi ya Watanzania waliopata chanjo ya kwanza kinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya Uviko19 nchini kujihakikishia wapo salama bila kutambua, kwa kushindwa kurudi kwenye vituo vya afya kuongezewa ya pili baada ya miezi sita.

Mratibu wa Chanjo kutoka Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Hezron Msongole, anafananua kuwa ni chanjo ya ziada iitwayo booster, kukabili maradhi Uviko 19.

Msongole anasema, takwimu zinaonyesha kuwa watu 313,269 wa Dar es Salaam, hawakurudi kwenye vituo vya afya kupata chanjo hiyo ya pili, baada ya kwanza kwa sababu ambazo hazijafahamika, akisema idadi hiyo ni tangu chanjo zilipoanza kutolewa mwaka 2021.

Anasema chanjo aina ya 'J&J' dozi ya kwanza walipatiwa watu 2, 271,698 na iitwayo 'Pfizer' walipata dozi 822,090, lakini waliorudi kupatiwa ya pili walikuwa 678,492, huku 143,598 hawakurejea.

"Chanjo ya Sinopharm dozi ya kwanza walikuwa 506,514, waliorudi dozi ya pili ni 410,057, watu 96,457 hawakurudi kukamilisha dozi ya pili, hii ni muhimu na ndiyo inakuwa na nguvu," anasema.

Kwa upande wa chanjo aina ya Sinovac, anasema dozi ya kwanza walichoma ni watu 327,876 na waliokamilisha dozi ya pili ni watu 275,007, watu 52,869 hawakurudi, chanjo ya Moderna dozi ya kwanza walipatiwa 70,501 na waliokamilisha ya pili ni 50,156 huku 20, 345 wakiwa hawajajitokeza.

Msongole, anasema pamoja na changamoto hiyo ya watu hao kutokamilisha chanjo ya pili, mkoa wa Dar es Salaam umevuka lengo la kitaifa, kwa kutoa chanjo kwa watu wengi nchini ikilinganishwa na mikoa mingine.

Anasema, awali walitarajia kutoa chanjo kwa watu 3,310,079, lakini wamevuka lengo kwa kuwapa 3,685,410.

"Kuchomwa chanjo ni bure, watu wanapaswa kuendelea kujitokeza kupata huduma hii, kwa kuwa inasaidia kupungua kusambaa kwa maambukizi mapya ya ugonjwa huu," anasema.

Anafafanua kuwa, chanjo za nyongeza zinaweza kutolewa kwa watu wote waliokamilisha dozi za awali, kipaumbele kikiwa ni wazee, watu wenye magonjwa sugu na wanaosafiri kwenda nchi zinazohitaji mtu awe amekamilisha chanjo zote.

Katika hilo, mdau Hidaya Sweid kutoka Asasi ya Mulika Tanzania, anasema serikali bado inapaswa kuendelea kuhakikisha taarifa sahihi zinawafikiwa wananchi na kuondoa uzushi na hisia potofu miongoni mwao.

"Inasemekana Uviko-19 bado ipo, sasa wizara ikitoa taarifa sahihi inasaidia wananchi kuwa na utulivu ama kuendelea kuishi kwa tahadhari, " anasema Sweid.

**WIZARA YA AFYA**

Wizara ya Afya katika taarifa yake ya Oktoba 22 mwaka jana kupitia Mpango wa Taifa wa Utoaji wa Chanjo, imeelekeza mwongozo wa utaratibu wanaopaswa kufuata watoa huduma za afya nchini kufanikisha lengo la utoaji wa chanjo ya dhidi ya UVIKO 19.

Watoa huduma hao wametakiwa kuweka rekodi maudhi yatokanayo na chanjo hizo ambayo mteja ameripoti katika rejesta ya UVIKO-19 kulingana na Mwongozo wa Mamlaka ya Taifa ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na visababishi vyake.

Pia, wametakiwa kutumia fomu maalumu za kutoa taarifa za maudhi hayo na kumpa taarifa mratibu wa chanjo kila siku.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, hadi kufikia Machi 15, mwaka jana watu 33,789 nchini walithibitika kuwa na UVIKO - 19 kati ya hao 803 walipoteza maisha kwa ugonjwa huo.

Wizara hiyo inabainisha kuwa hadi kufikia Machi 12, mwaka jana, watu 2,820,545 wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea wamepata chanjo kamili dhidi ya ugonjwa huo.

Idadi hiyo ni sawa na asilimia 9.17 ya Watanzania 30,740,928 wa kuanzia umri huo wanaokidhi vigezo vya kupata chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

Hata hivyo, idadi hiyo bado inatajwa hairidhishi kufikia kinga ya jamii ambayo inapaswa kufikia angalau asilimia 70 ya watu kuanzia umri huo wa miaka 18 na kuendelea.

Chanjo dhidi ya virusi hivyo imekuwa ikitolewa kwenye hospitali za serikali na vituo maalumu vilivyotengwa kwa ajili hilo.

## SAMIA ANAIJENGEA WILAYA HOSPITALI HADHI YA MKOA NA ZAWADI ZAHANATI, VITUO AFYA

**Inatoka Uk. 11**

mfupi mwaka huu, kitaanza kazi.

Kwa mujibu wa Dk. Katwale, mageuzi hayo kunawaondolea wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya, ikiwamo upasuaji katika Hospitali ya Muriti na wilayani, Nansio, mgonjwa wa Igalla alilazimika kusafiri kilomita 23.

Anaeleza, kwa sasa kituo hicho kinahudumia wagonjwa wa nje (OPD) na kliniki (RCH). Tatizo lililokuwapo awali ni uhaba wa maji, hata wajawazito wakatakiwa kwenda na maji hospitali au kuyafuata mtoni.

Mganga Mfawidhi anasema kukamilika mradi tajwa, kunasaidia kupatikana maji ya kutosha, tofauti na zamani; sasa kuna maji ya kudumu misimu yote, ikitumika teknolojia ya kuvuna maji ya mvua, kisha yanahifadhiwa.

Anaeleza, mwaka huu kituo hicho kilipokea Sh. shilingi milioni 49.9 za kujenga miundombinu ya kuchoma taka, shimo la majivu na shimo la kondo la nyuma.

Mengine anataja ni sehemu ya kunawa mikono, mnara wa kuhifadhia tanki la maji lita 5000, kupanua chumba cha wajawazito kujifungua, ujenzi wa tanki la maji lita 50,000 la kuhifadhi maji yanayovunwa kwa mvua, vimekamilika.

"Mpaka sasa kituo hili kimegharimu milioni mia 518, kupitia mradi wa WASH. Ttumeweza kuondokana na tatizo la uhaba wa maji, hiyo ni baada ya kujenga tanki la chini lenye ujazo wa lita 50,000, kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua, Dk. Katwale akinena, wanawake wengi sasa wanafika hapo kwa wingi kujifungua.

Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi mwaka jana, Wilaya ya Ukerewe ina jumla ya wakazi 387,815, sehemu kubwa ni vijana na Watoto, wanaiohudumiwa kiafuia na serikali, kupitia zahanati 28, vituo va afya 24, huku kiukiwapo vine vipya, wanaoisji katika vijiji 76 na vitongoji 514 na visiwa 38.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Igalla, Obedi Mkingila, anasema kukamilika na kuanza kutumika Kituo cha Afya Igalla, kunaondoa adha kwa wananchi Igalla, kutumia usafiri pikipiki kufuata huduma za afya katika Kituo cha Afya Muriti.

"Kinamama wajawazito wanapata changamoto kutembea umbali mrefu hadi kituo cha afya Muriti... tunasubiri kwa hamu kuona kinaanza kufanya kazi" anaesema mkazi wa Igalla, Nyakwesi Katula.

Mganga Mkuu Wilaya ya Ukerewe, Dk. Mkombe, anataja maendeleo na furaha ya umma katika miaka miwili iliyiopita, serikali imejenga zahanani mpya nane na vituo vitatu vya afya, katika wilaya hiyo inayozungukwa na maji.

"Lengo la serikali ni huduma kumfuata mwananchi aliko na siyo wananchi kufuata huduma mbali, kwani dharura inaweza kutokea hasa majira ya usiku na wakashindwa kupata huduma kwa wakati.

"Pia, tuna 'ambulance' (gari la wagonjwa) za boti mbili na tuko kwenye mpango wa kuongeza nyingine, ili kutoa huduma za dharura visiwani" anasema Dk. Mkombe

**MKURUGENZI AFUNGUKA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ukerewe, Emmanuel Shelembi, anasema wamepokea shilingi bilion 5.1 za kujenga na kukabati vituo vya afya.

Anaorodhesha vituo vipya vilivyokamilika ni; Igalla, Murutilima na Ilugwa, huku ujenzi wa zahanati za Buguza na Ghana, zikitarajiwa kukamilika, kuuondolea adha wananchi ya kufuata huduma umbali mrefu, hasa wakazi wa visiwani.

Anaeleza, serikali sasa inaendelea na maboreshe kwenye Hospitali ya Bwisa, jengo la wagonjwa mahututi (ICU) lialogharimu shilingi milioni 250, pia nyumba za watumishi watatu katika Kituo cha Afya Kagunguli, ikiwa na thamani shilingi milioni 90.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, pia kunakarabatiwa vituo vya afya 24 na kuimarishwa upatikanaji dawa na vifaa tiba.

"Visiwa 15 kati ya 38 vya wilaya ya Ukerewe vinakaliwa na watu, hivyo lengo la serikali ni kufikisha huduma kwa wananchi katika visiwa hivyo na kuwaondolea adha ya kutumia vivuko kufuata huduma hizo" anaeleza Shelembi.

**UONGOZI WILAYA**

Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Hassan Bomboko, anaeleza serikali kuu imewezesha kupata miradi mikubwa, pia vifaa vya kwenye baadhi ya hospital za wilaya hiyo, huduma kwa wananchi ikiboreka.

Mganga Mkuu Wilaya ya Ukerewe, Dk. Charlse Mkombe, anaeleza maelezo yaliyoko katika utawala wa Rais Dk. Samia ni kwamba: "Huduma kumfuata mwananchi aliko na siyo wananchi kufuata huduma mbali, kwani dharura inaweza kutokea hasa majira ya usiku na wakashindwa kupata huduma kwa wakati.

Pia tuna 'ambulance' za boti mbili na tuko kwenye mpango wa kuongeza nyingine, ili kutoa huduma za dharura visiwani," anaeleza Dk. Mkombe

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe Joshua Manumbu, anaeleza vituo vyote vya afya sasa, vimejengwa kwa ubora mkubwa. siri yake ni ushirikiano uliopo baina yao na ushirikishwaji mzuri wa wananchi, matarajio yao ifikapo Desemba ijayo vituo vyote vya afya vitaanza kutoa huduma na vifaa vitakuwa vishafika.

AFYA

# Ukweli wa kansa inavyotibika, undani kutoka kwa aliyekatwa titi kudhibiti

Na Restuta James

UKIKUTANA naye ni ngumu kumtambua ana changamoto ya maradhi. Sura yake yenye nuru na ukaribisho wa tabasamu. Huyo ni Jasmin Said, mama kijana mwenye maisha ya kawaida kama wengine.

Jasmin, mwenye umri miaka 33, yuko katika tiba ni shujaa wa saratani. Alibainika kuwa na maradhi hayo miaka mitatu iliyopita, akakatwa titi moja.

Akizungumzia safari yake ya ugonjwa hadi kuwa shujaa, Jasmin anasema siku moja aliona ana uvimbe kama gololi kifuani ambao hakikuwa kinauma.

"Nilivyokiona sikuridhika nacho, kesho yake nikaamkia zahanati ambako daktari aliniandikia dawa za wiki mbili za kuyeyusha uvimbe. Wiki ya tatu nikasikia kitu kinaniambia 'hebu minya chuchu', nilivyominya nikaona inatoa majimaji ambayo ni mazito kama rangi ya mafuta ya kula," anasema.

Jasmin anasema, kadri siku zilivyozidi kuendelea, chuchu ilianza kutoa damu ambayo ilimshtua, japokuwa hakuwaza kama inaweza kuwa ni saratani.

"Nilihisi kile kiuvimbe kilikuwa ni jipu, kwa hiyo limepasukia kwenye ziwa, hata sikurudi hospitali. Ziwa likaendelea kutoa damu hata bila kukamuliwa nikafikia hatua ya kulala na brazia; nikiamka imelowa, nikiingia bafuni kuoga damu zinatoka. Hali hiyo sikuridhishwa nayo, mwenzangu (baba mtoto wake), akaniambia niende hospitali," anasema.

Anafafanua kwamba, akaenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke, ambako baada ya vipimo alibainika kuwa na uvimbe na madaktari wakamshauri afanyiwe upasuaji, tiba ambayo haikumridhisha, kwani mwenza wake alitafuta taarifa za dalili za saratani na kumshauri kwenda Taasisi ya Saratani Ocean Road.

Jasmin anasema baada ya wiki moja, akaenda Ocean Road alikofanyiwa vipimo na baada ya vipimo, daktari akamrudisha Temeke kwa barua ya maombi ya kumkata kinyama, ili kifanyiwe uchunguzi wa kina katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na majibu yarudishwe Ocean Road.

"Nilifanya kama daktari alivyoelekeza...sikusomewa majibu Muhimbili. Nilivyoyapokea niliyapiga picha, nikawatumia baadhi ya madaktari ambao wengine walinificha. Daktari mmoja mwanamke nilimuomba aniambie ukweli, akaniambia Jasmin una saratani naomba kesho uende Ocean Road," anasema.



Jasmin Said; shujaa anayepambana na kansa. **PICHA ZOTE: RESTUTA JOSEPH.**

Jasmin anasimulia kilichofuara: "Nilishtuka na kulia sana, sikuamini! Nikampigia simu mwenzangu (mumewe) kumpa majibu, akakata simu akaniambia anakuja. Nililia nikijua maisha yangu ndio basi tena. Namshukuru Mungu mwenzangu alinipa moyo sana, hadi niliamka pale kama siumwi."

Anasema, kesho yake, akaamkia kwenye hospitalini Ocean Road, ambako daktari akamsomea majibu na kumthibitishia ana saratani. Anasema hakutetereka, kwa kuwa alishatiwa moyo kisaikolojia nyumbani.

"Madaktari waliitana kama watatu hivi, wakaniangalia ziwa na kunishauri nikatwe, kwa sababu kwa umri wangu ugonjwa ungesambaa sana. Hili lilinishtua mno, kwa sababu sikutegemea kabisa kukatwa ziwa," anaeleza.

Jasmin (33), mama wa mtoto mmoja mwenye wa miaka sita, anasema alirudi nyumbani akiwa mnyonge na aliyepoteza tumain, lakini mwenza wake akamsihi kukubali tiba hiyo, kwani wako watu wanaopoteza viungo vikubwa zaidi ya titi.

Jasmin anasema, safari yake ya tiba ilianza rasmi Juni 14, 2023 alipokatwa titi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na baada ya wiki moja, alihamishiwa ORCI.

"Nikaanza mzunguko wa 'chemo' (tiba kemia), nikaingia kwenye mionzi na sasa ninatumia dawa za homoni. Namshukuru sana Mungu naendelea vizuri," anasema.

Hata hivyo, anasema tiba kemia ilimsababishia kutapika kupita kiasi, hadi familia ilimzuia kuendelea nayo, lakini walivyompa nafasi ya kuamua, akaomba arudishwe Ocean Road.

"Namshukuru Mungu nilimaliza 'chemo' zote nane, nikaingia kwenye mionzi ambayo nilipiga 16, nilipata vidonda, lakini nilipambana mpaka nikamaliza matibabu na Februari mwakani nitatimiza miaka miwili tangu nilipomaliza matibabu," anasema Jasmin.

Anasimulia alipomaliza tiba mionzi, akaanza dawa za kurekebisha homoni anazoendelea nazo, huku akihudhuria kliniki katika taasisi hiyo.

Shujaa mwingine wa saratani ya matiti aliyekatwa titi la kushoto, Stella Mbonde, anasema aligundulika kuwa na maradhi hayo miaka 22 iliyopita na kueleza kuwa saratani inatibika, kama itagundulika katika hatua za awali.

Stella anawasihi wananchi kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara ili iwe rahisi kubaini ugonjwa mapema kabla haujasambaa na kushindwa kutibika.

**TIBA SHUFAA ORCI**

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo ya saratani nchini, Dk. Julius Mwaiselage, anasema mbali ya tiba za kisayansi, hospitali inatoa tiba shufaa inayoundwa na timu daktari, muuguzi, mfamasia, ustawi wa jamii, mwanasaikolojia, mtaalamu wa lishe na watu wa huduma za kiroho.

"Tiba shufaa ni maalumu kwa ajili ya kuimarisha maisha ya mgonjwa, kimwili, kiakili na kiroho ili aweze kuishi vizuri wakati wote wa kuugua," anasema.

Dk. Mwaiselage anafafanua tiba shufaa, kwamba inaambatana na utoaji dawa ya maumivu, aina ya 'Oral Morphine', inayomwondolea maumivu mgonjwa wa saratani aliye katika hali ya juu ya ugonjwa.

"Kubwa katika tiba shufaa ni utoaji wa dawa za maumivu, tunafahamu wagonjwa wengi hasa wa muda mrefu wanapata maumivu na ndicho kinachofanya maisha ya mgonjwa yasiwe bora. Oral Morphine, ni maalumu kabisa kuondoa maumivu ya aina yoyote," anasema.

Anafafanua, kabla ya mgonjwa kupewa dawa hiyo, huanza na dawa za awali ambazo zisipopunguza maumivu kwa kiwango kinachotakiwa, huanza dozi hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage.

Dk. Mwaiselage anasema Tasisi ya Saratani (ORCI), inatoa dawa hiyo, kwa kuwa wagonjwa wengi wa saratani wanafika hospitalini, wakiwa katika hatua za juu za ugonjwa, inayoambatana na maumivu makali.

"Moja ya jukumu la tiba shufaa ni kuhakikisha mgonjwa hapati maumivu. Kwa hiyo, dawa maalum ipo kama nilivyosema na tunaitoa kwa wagonjwa wenye uhitaji huo," anasema.

Anasema taarifa za jarida la kitafiti la Lancet, inaeleza kuwa takribani watu milioni 25 walifariki mwaka jana wakiwa katika maumivu makali na tiba ya Oral Morphine, inalenga kuhakikisha mgonjwa hapati maumivu hata anapokuwa katika hatua za juu za ugonjwa.

Mtaalamu huyo anasema kila mwaka, Ocean Road, inahudumia wagonjwa 65,000 na mwaka jana 46,061, kati yao waliingia kwenye mpango wa tiba shufaa.

Dk. Mwaiselage, anasema kati ya asilimia 60 hadi 70 ya wagonjwa, walifika kwenye taasisi hiyo, wakiwa katika hali ya juu ya ugonjwa na kwamba, ndio maana wametoa kipaumbele cha dozi ya Oral Morphine.

Kwa mujibu wa daktari huyo, dawa hiyo inaweza kutolewa kwa wagonjwa wa ajali, kisukari na akili; walio katika maumivu makali.

Dk. Mwaiselage anasema, kumekuwapo ongezeko la wagonjwa wapya kutoka 1,500 mwaka 2000 hadi 8,000 mwaka jana.

Daktari bingwa wa Saratani, Dk. Faraja Kiwanga, anasema, hospitali hiyo pia inatibu saratani kwa mionzi, kemia, upasuaji, vichocheo na dawa za kupunguza maumivu.

Mkurugenzi wa Uuguzi na Muuguzi Bingwa wa Tiba Shufaa, Mary Haule, anataja changamoto zinazowakabili wagonjwa wa saratani, zikiwamo za kisaikolojia, wakihofia tiba na uwezekano wa kupona.

"Kuna wengine ni vijana, wengine ni wazazi ambao wana wategemezi nyuma yao. Wengi wanapopata saratani wanajiuliza 'nimemkosea ni Mungu', ndio maana kwenye tiba shufaa, tunakaa nao kuwaweka sawa," anasema.

"Kwenye tiba shufaa tunaanza kumhudumia tangu anapopokea majibu ya ugonjwa, tunampa faraja kwa lengo la kuboresha maisha ya mgonjwa na familia yake," anafafanua.

Kwa mujibu wa taarifa za Taasisi ya Saratani Ocaen Road, saratani inayoongoza nchini na asilimia yake kwenye mabano ni; shingo ya kizazi (35), matiti (15), njia ya chakula (10), ngozi (9), muunganiko wa saratani ya kichwani, mdomoni na shingoni (8), tezi dume (7) na utumbo mpana (6).

AFYA

## MAJIBU YA MMAM KITAIFA…

# Rais Samia:Vifo vya uzazi vimepungua 80%, kusuasua wenye chini ya miaka 5

•Akumbuka alichozindua'Jiongeze Tuwavushe Salama,'...



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa katika ziara ya kikazi hospitalini, akihimza serikali yake kuwekeza zaidi kwenye huduma za dharura na kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi na watoto wachanga. **PICHA: MAKTABA**

**Na Yasmine Protace**

KUBORESHWA kwa huduma za afya nchini na hasa katika miaka 15 ya kuwapo kwa Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM), kunatajwa kumesaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi nchini.

Kujifungua salama, kiimani ni baraka za Mungu, huku serikali nayo ikijipanga kutia MMAM, kunuia kupunguza vifo hivyo vitokanavyo na uzazi nchini.

Awali baadhi ya wajawazito kutoka maeneo mbalimbali walikuwa wakiripotiwa kufariki dunia kutokana na changamoto za uchache na ufanisi wa huduma za vituo vya afya.

Kukashuhudiwa kihistoria nchini katika awamu sita za uongozi, changamoto hizo kwa kila kiongozi aliyekuwa madarakani kwa kipindi chake, akihakikisha huduma za afya zinaboreshwa kwa hatua yake ya maendeleo, ili kuwawezesha wajawazito na watoto kuwa salama.

Itakumbukwa, MMAM ni sehemu ya miradi ya awali aliyoanza nayo Rais Jakaya Kikwete, katika awamu ya nne na ikaendelezwa na kuboreshwa na waliopokea kijiti chake, hadi sasa takwimu tajwa za maboresho kiafya leo, ni zao lake.

Hatua mojawapo inayoshuhudiwa, ni kuwapo idadi ya kutosha ya vituo afya vya kuwahudumia wananchi, ndani yake ikikabiliwa changamoto za utaalamu, wataalamu na vifaa, ambayo imekuwa ikiongezeka kutokana na ongezeko la vituo hivyo.

Kwa mujibu wa MAMM, muundo wa afya kunakuwapo hospitali ngazi ya taifa, ambayo ni Muhimbili ikisaidiwa na Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete zote za Dar es Salaam, hali kadhalika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma.

Hivi karibuni, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema kuwa jitihada za kuboresha huduma bora za afya, zimesaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Anarejea mageuzi ya takwimu, vifo hivyo sasa viko katika wastani wa 530 kwa kila vizazi hai 100,000 katika mwaka 2015/16 na vimepungua hadi kufikia 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

Ni kauli ya Rais Dk. Samia katika uzinduzi wa Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria ya Mwaka 2022, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

"Hii ni hatua kubwa, kiwango hiki kimepungua kwa asilimia 80,

> **"Shabaha ya malengo endelevu ya dunia ya mwaka 2030, inaelekeza kupunguza vifo vya mama wakati wa uzazi na visizidi 70 kwa kila vizazi hai 100,000. Sasa, hivi tupo 10, safari yetu mpaka mwaka 2030 tunaweza kufikia hii shabaha," anatamka Rais Dk. Samia.**

Mwenyezi Mungu atuwezeshe tuendelee kupunguza na tunaona jitihada zinazofanywa kwenye sekta ya afya zinaleta matokeo chanya" anasema.

Rais Dk. Samia anarejea kwenye miongozo ya imani kwamba, hadi sasa serikali ina wajibu wa kujipanga kutoa huduma bora za afya kwa wananchi na kuwekeza zaidi kwenye upatikanaji vifaa, ili wananachi waweze kutoa huduma bora.

"Shabaha ya malengo endelevu ya dunia ya mwaka 2030, inaelekeza kupunguza vifo vya mama wakati wa uzazi na visizidi 70 kwa kila vizazi hai 100,000. Sasa, hivi tupo 10, safari yetu mpaka mwaka 2030 tunaweza kufikia hii shabaha," anatamka Rais Dk. Samia.

Anaongeza kwa kuhimiza mwelekeo wa Tanzania sasa ni mzuri, hivyo madaktari, wauguzi na wakunga wasibweteke, bali wakaze mwendo na vifaa vipo, wakafanya kazi ya kuokoa uhai wa umma.

Kuhusu vifo vya watoto wenye umri chini ya umri wa miaka mitano, anahimiza kuwa vifo vya watoto hao vimepungua kutoka 67 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia vifo 43 kwa kila vizazi hai 100,000.

Katika hilo, Rais Dk. Samia anawataka watendaji na wadau wa sekta ya afya waongeze kasi ya uwajibikaji na kupunguza vifo vya watoto wachanga, ambavyo afafanua kuwa ripoti inaonyesha vifo hivyo vimepungua kwa asilimia moja.

"Ikumbukwe kuwa mnamo mwaka 2018 nikiwa Makamu wa Rais, nilizindua kampeni ya 'Jiongeze Tuwavushe Salama,…" anatamka akiongeza:

"Ililenga kuhimiza uwajibikaji wa viongozi na watendaji ndani ya Sekta ya Afya, kushughulikia changamoto za afya ya uzazi, mama na mtoto, ili kuweza kufikia malengo endelevu ya 2030 pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto za afya ya uzazi."

**WAZIRI UMMY**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anafafanua juhdi za kiserikali katika miaka miwili sasa, chini ya utawala wa Awamu ya Sita, kwamba serikali imejenga vituo vipya vingi vya kutoa huduma nchini kote, akifafanua:

"Ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, jumla ya vituo vipya 1,498 vya kutoa huduma za afya vimejengwa hapa nchini."

Waziri Ummy, mzoefu wa Wizara ya Afya, anarejea historia nchi ilikotokoa, kwamba: "Mwaka 2021 tulikuwa na vituo 10153 leo tuna vituo 11651, ongezeko la vituo 1498 na vingi vimeanza kufanya kazi."

Pia anataja namna Dk. Samia amewezesha ununuzi na usimikajii wa vifaa tiba vya kisasa, zikiwamo mashine za uchunguzi wa radiolojia za aina ya 'CT Scan' kusambazwa nchini kote.

"Leo hii hakuna haja tena ya mtu kutoka Kigoma au Katavi kusafiri hadi kuja Dar es Salaam kwa ajili ya huduma za 'CT Scan'. Haya yote umewezesha wewe Rais Samia," anasema Waziri Ummy.

Hadi sasa, mbali na kuongiozwea idadi ya zahanati, vituo vyua afya na hospitali, penu7e uhitajj, katika ngazi ya kiataifa hospitali kama Bejamin Mkapa ya makao makuu Dodoma, pia MOI, Muhimbili - MNH na Jakaya Kikwete, zote za Dar es Salaam, zimekuwa zikiongeza stadi mbalimbali za ubunifu katika tiba, kwa mafunzo wanayopata nje ya mipaka.

Ubunifu huo unasambazwa katika hospitali za kanda na mikoa, madaktari hao wa juu kwenda kufunza huko, ili ujuzi na huduma kuwafikia iwafikie Watanzania wengi zaidi mahali waliko.

Katika hilio, Rais Dk. Samia, amekuwa akitoa ushirikiano wa kugharamia mafunzo, pia kunua vifaa hitajika, sasa Tanzania imekuwa kivutio ca kujifunza na katika baadhi ya matukio, kwrnda kuhudumia nchi jarani, kama vile Malawi, hivi karibu Rwanda.

Ni hatua amabayo hata katika dilomasia, imefungaui uvinvu unaoitwa Utalii Tiba, mataifa Jirani ya ayofika nchini kupata huduma hiyo, ambayo nchi nyingi za Kiafrika zinafuata katika nchi za mbali.



# Jafo awataka wafugaji kufuga kwa tija kuepuka uharibifu mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amewataka wafugaji nchini kuhifadhi mazingira kwa kufanya shughuli za ufugaji wenye tija kwa maendeleo endelevu.

Dk. Jafo aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa wiki ya maonesho ya ufugaji wenye tija na utunzaji wa mazingira sanjari na kuzindua Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania (CHAMAUTA), jijini hapa.

Alisema ufugaji endelevu usioathiri hifadhi ya mazingira utasaidia kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji nchini.

"Tuepuke migogoro baina ya wakulima na wafugaji ambayo tunashuhudia ikitokea katika baadhi ya mikoa nchini husababisha kutoelewana kwa makundi haya mawili hali inayoweza kusababisha uvunjifu wa amani, na tuna wajibu wa kulinda amani," alisisitiza.

Aidha, alihimiza wafugaji ambao wamepata ufadhili kutumia fursa ya mkutano wa 28 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabdiliko ya Tabianchi (COP 28), kushiriki kikamilifu katika mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Novemba 28 hadi Desemba 5, 2023 utakuwa ni adhimu ya kuitangaza Tanzania inavyofanya ufugaji rafiki wa mazingira.

Waziri Jafo alitoa wito kwa CHAMAUTA kulitumia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kupata uelewa kuhusu kanuni zinazosimamia mazingira ili kuepuka uharibifu.

# Tz yafikia malengo sifuri 3 kutokuwa vifo vya Ukimwi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imefikia malengo ya kitaifa ya sifuri tatu yaani kutokuwa na maambukizi mapya, kutokuwa na unyanyapaa na ubaguzi, na kutokuwa na vifo vitokanavyo na Ukimwi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kukamilika kwa utafiti wa viashiria na matokeo ya Ukimwi nchini Tanzania wa mwaka 2022/23.

Alisema utafiti huo unaonesha maambukizi mapya yamepungua ikilinganisha na mwaka 2016/17 na kwamba matokeo ya kina ya utafiti huo yatatangazwa Desemba mosi, 2023 katika Siku ya Ukimwi Duniani.

"Uchakataji wa takwimu zilizokusanywa unaendelea na Taarifa ya Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya VVU na Ukimwi ya mwaka 2022/23 itazinduliwa rasmi tarehe 1 Desemba, 2023," alisema.

Alisema taarifa ya awali inaonesha kuwa, Tanzania imepata matokeo chanya katika mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi na idadi ya maambukizi mapya inaendelea kupungua ikilinganishwa na matokeo ya utafiti wa mwaka 2016/17.

Alifafanua kuwa utafiti huo hufanyika kila baada ya miaka mitano na mara ya mwisho ulifanyika mwaka 2016/17, lengo la utafiti huo ni kupima matokeo ya juhudi za mapambano dhidi ya Ukimwi.


Alibainisha kuwa kupitia utafiti huo watapata taarifa kuhusu viashiria na matokeo ya VVU/Ukimwi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2022/23 ambazo ni takwimu muhimu kuhusu hali ya Ukimwi nchini.

"Utafiti wa mwaka 2022/23 ni wa tano kufanyika nchini Tanzania kupima mwenendo wa VVU na Ukimwi duniani, kwa kupima kiwango cha maambukizi mapya na kufubaa kwa VVU katika ngazi ya jamii," alisema.

Alisema utafiti huo umefanywa na serikali kupitia Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Tume ya Kudhibiti Ukimwi Zanzibar (ZAC), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar (OCGS) kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya serikali zikiwamo Kituo cha Kudhibiti Magonjwa na Kinga (CDC) na Chuo Kikuu cha Columbia (CAP), kutoka nchini Marekani.

"Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP) na Mpango Jumuishi wa kupambana na Ukimwi, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma, kazi hii imefanyika kwa ufadhili wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kudhibiti Ukimwi (PEPFAR)," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi kupokea taarifa hiyo ya awali na kujiandaa kupokea matokeo rasmi ya utafiti huo ifikapo Desemba mosi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Mbunge wa Same Magharibi, David Mathayo David (katikati) na Mbunge wa Viti Maalum, Zainab Katimba, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Wanafunzi watahadharishwa mapenzi na walimu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANAFUNZI wapya waliochaguliwa kujiunga na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Kampasi ya Singida kwa msimu wa masomo wa 2023/24, wametahadharishwa kutojihusisha na uhusiano wa kimapenzi na walimu kwa lengo la kupewa matokeo mazuri ya mitihani.

Kaimu Mkurugenzi wa kampasi hiyo ambaye ni Mratibu wa Taaluma, Flora Lemnge, alibainisha hayo juzi katika semina elekezi kwa wanafunzi hao na kueleza kuwa mwanafunzi atakayejihusisha na uhusiano wa kimapenzi na mwalimu ili kujaziwa matokeo mazuri kwenye mitihani yake itakuwa imekula kwake.

"Nasimama kama mama, nafasi yangu ya kitaaluma naiacha kwa muda 'ewe binti usivue nguo zako kisa upate mtihani itakula kwako' kuna baadhi yenu mmekuja hapa na kuanza kujipangia walimu baada ya kuona ana mshahara na yupo 'smart' atakukula bure kwani mtihani huo ni uleule utashindanishwa na wenzako wa kanda zingine na unasahihishwa na walimu wa ndani na wa nje na si vinginevyo," alisema.

Lemnge alisema utaratibu wa usahihishaji wa mitihani ni kukusanywa na kusahihishwa sehemu moja na hakuna mwalimu anayesahihisha darasa alilofundisha anapangiwa darasa lingine na kila darasa anasahihisha mwalimu mmoja hivyo asije akatokea mtu na kukueleza kuwa atakufelisha.

Aidha, Lemnge aliwataka wanafunzi hao kuzingatia sheria zote za taasisi hiyo na nchi na kuhudhuria masomo kwa kuwa hilo ndilo jambo walilolikusudia wakizingatia kuwa wazazi wao wamekuwa wakitoa fedha nyingi kwa ajili yao.

Alisema lengo la semina hiyo ni kuwafanya wanafunzi hao wazijue taratibu zote za taasisi hiyo ikizingatiwa kuwa kila mmoja ametoka katika mikoa mbalimbali na tabia tofauti.

Mshauri wa wanafunzi TIA, kampasi ya Singida, Ambwene Kajula, aliwapongeza wanafunzi kwa kuchagua chuo hicho na kuwashuru wazazi kwa wanavyojitoa kuwasomesha watoto wao.

Alisema baadhi ya mambo yanayofundishwa katika semina hiyo elekezi ni kutaka kuwaonesha wanafunzi hao mazingira watakayokuwa nayo na jinsi ya kuishi kufikia malengo waliyoyakusudia na watafundishwa mambo ya aina mbalimbali kama miongozo, sheria na kanuni ambazo wanatakiwa kuzifuata wakiwa katika taasisi hiyo.

Aidha, Kajula alisema pia watawakutanisha na wadau kama Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), watu wa dawati la jinsia, NSSF, NHIF na Taasisi za kifedha kama mabenki, vyombo vya mawasiliano ya simu na kuwafundisha mbinu mbalimbali za kimaendeleo.

Kwa upande wake Mratibu wa Mipango na Dawati la Malalamiko wa taasisi hiyo, Magreth Emmanuel, aliwataka wanafunzi hao wanapokuwa na changamoto mbalimbali kuziwasilisha kwa serikali ya wanafunzi wa chuo hicho.



# H'shauri yatishia kutozoa taka taasisi za serikali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imetishia kusitisha uzoaji wa taka kwenye baadhi ya taasisi za serikali vikiwamo vyombo vya dola kutokana na taasisi hizo kutolipa ada ya taka kwa zaidi ya miaka sita huku wakiendelea kupata huduma.

Madiwani wa halmashauri hiyo waliibua kero hiyo juzi kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Badiwani na kuzitaja baadhi ya taasisi hizo kuwa ni Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) ambayo inadaiwa zaidi ya Shilingi milioni saba.

Diwani wa Kata ya Mbalizi Road, Adam Simbaya alisema taasisi hizo zimewekewa kiwango cha kuchangia Sh. 100,000 kila moja, ambacho hakiendani na wingi wa taka zinazozalishwa, lakini bado hazilipi.

Alisema utaratibu wa ulipaji wa ada ya taka ni kila kaya inatakiwa kulipa, lakini kwenye taasisi hizo utaratibu uko tofauti kwa maelezo kuwa wamewekwa kwenye hesabu moja.

Alisema baadhi ya taasisi hizo ambazo zipo kwenye kata yake waliamua kuacha kuondoa taka hizo, lakini maofisa wake wanafanya mazungumzo na wakuu wa idara ya mazingira wa jiji na kuziondoa taka hizo.

"Sisi pale kwenye ofisi yetu ya kata tulishindwa kulipia maji watu wa mamlaka ya maji wakaja wakakata, sasa kwanini na sisi tusichukue hatua ya kusitisha kuziondosha taka kwenye maeneo yao ili tuone kama hawatalipa," alihoji Simbaya.

Alisema kaya za maaskari wanaoishi kwenye kata yake zipo zaidi ya 400, lakini wanatakiwa kulipa 100,000 pekee na kusisitiza huduma hiyo isitishwe.

Diwani wa Kata ya Isyesye, Ibrahim Mwampwani, alisema baadhi ya taasisi za umma zinalipa ada hiyo kwenye kata husika bila vikwazo na kutaka na taasisi hizo ambazo hazilipi zichukuliwe hatua.

Alisema Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa taasisi za serikali zinazolipa ada hiyo bila tatizo na taka zinaondolewa kwa wakati.

Alisema taasisi ambazo hazilipi ada hiyo zinasababisha bajeti za kata husika kuvurugika na kushindwa kutekeleza vizuri majukumu yake hasa ya uondoshaji wa taka.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, John Nchimbi, alisema wanakusudia kuanza kuchukua hatua dhidi ya taasisi hizo ikiwa ni pamoja na kuzikumbusha kulipa kabla hatua zingine kali zaidi hazijaanza kuchukuliwa.

Alisema wanakusudia kuanza kwa kuziandikia barua ya kuzikumbusha madeni yao na kuzipatia muda wa siku 30 kulipa madeni ambayo zinadaiwa.

"Kama watashindwa kulipa madeni hayo ndani ya siku hizo 30 tutachukua hatua za kusitisha huduma kwenye maeneo yao kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza kuzilipia fedha hizo," alisema Nchimbi.

Naibu Meya wa Jiji la Mbeya, Kefas Mwasote, alisema miaka ya nyuma zilikuwepo taasisi nyingi ambazo zilikuwa hazilipi ada hiyo na kwa sasa zimebakia chache kwa maelezo kuwa zingine zililazimishwa kulipa.



Mtafiti Udongo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Fedrick Mlowe (kushoto), akiwaonyesha baadhi ya wakulima shamba ambalo limewekwa chokaa kwa ajili ya kupunguza tindikali kwenye udongo ambayo ni mbinu inayotumika kurejesha rutuba kwenye udongo ulioathiriwa na tindikali, walipotembelea kituo hicho jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Madiwani waipongeza TARURA kujenga barabara viporo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Mji Njombe, limepongeza Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), wilaya ya Njombe kwa utekelezaji wa barabara viporo ambazo waliagizwa baada ya miezi mitatu ziwe zimekamilika.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji ya Njombe, Erasto Mpete, wakati wa mkutano wa robo ya kwanza ya Baraza la Madiwani la halmashauri hiyo.

Mpete alisema Baraza la Madiwani limeridhishwa na utekelezaji ambao umefanyika kwenye barabara viporo zote.

"Sambamba na hilo nimuombe meneja wa TARURA barabara nyingine zikarabatiwe, ikizingatiwa kipindi cha kuelekea kwenye mvua maana yake ni kama mwezi mmoja au miwili, tuombe utekelezaji wa barabara nyingine uende kwa kasi, lakini pia tuangalie barabara zilizo muhimu," alisema Mpete.

Wakati huo huo, Mpete alimuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Kuruthum Sadick, kuwaondoa machinga wote wanaouza mali mbichi sehemu ambazo sio rasmi na kwenda katika soko la Joshoni.

Mpete alisema changamoto iliyokuwa inasababisha wafanyabiashara wasiamie katika soko hilo ni ubovu wa barabara. "Changamoto kubwa ilikua ni barabara ya lami,wakati wa mvua magari ilikuwa ni changamoto kwenda sasa barabara ya lami imetengenezwa ni jukumu letu sasa kuhakikisha lile soko linaanza kufanya kazi mara moja." alisema Mpete.

# TARI yakabidhi kilo 200 mbegu bora za pareto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini hapa, imekabidhi zaidi ya kilo 200 za mbegu bora za pareto kwa Serikali ya Mkoa wa Songwe kwa ajili ya kugawa kwa wakulima wa wilaya za Ileje na Mbozi ili kuongeza uzalishaji.

Miche hiyo ilikabidhiwa juzi na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Denis Tippe, ambaye alimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael.

Alisema mbegu hizo zina uwezo wa kuzaa maua mengi tofauti na za asili.

Alisema ilitoa Sh. milioni 200 kwa kituo hicho kwa ajili ya kufanya utafiti wa mbegu bora za pareto na mbegu zilizoanza kusambazwa ni sehemu ya utafiti huo.

Alisema kwenye utafiti waliofanya walizalisha tani mbili za zao hilo ambazo zina uwezo wa kutosheleza wakulima 18,000 wa maeneo yote ambayo yanazalisha zao hilo.

"Tunaishukuru serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kutupatia fedha hizo, hii ni mara ya kwanza serikali inafanya hivyo, ni hatua nzuri na tunaamini tija itaongezeka sana," alisema Dk. Tippe.

Aliwataka wananchi kuachana na mbegu za asili walizokuwa wamezoea kuzitumia na waanze kutumia mbegu hizo za kisasa ili kuongeza uzalishaji utakaosaidia hata kipato chao kuongezeka.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Ileje, Helman Njeje, alisema wilaya hiyo ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa zao hilo katika Mkoa wa Songwe na ni miongoni mwa mazao makuu ya biashara ambayo yanazalishwa.

Alisema watahakikisha wanawahamasisha wakulima hao kuanza kutumia mbegu hizo za kisasa kwenye kilimo cha zao hilo kutokana na kufanyiwa utafiti na zina uwezo wa kuzaa maua mengi kuliko zile za asili.

Alisema lengo la wilaya hiyo ni kulifanya zao hilo kuwa miongoni mwa mazao yanayolimwa zaidi na wananchi kutokana na hali ya hewa kuruhusu.

"Tunawashukuru wataalamu hawa kwa kutupatia mbegu hizi, kwa kiwango kikubwa mbegu hizi zinaelekezwa katika Wilaya yetu ya Ileje, msimu wa kupanda ukianza tutapita maeneo yote ya uzalishaji kuwapatia wananchi elimu ili wachangamkie mbegu hizi za kisasa," alisema Njeje.

Akipokea mbegu hizo, Mkuu wa Mkoa wa songwe, Dk. Francis, aliwaagiza maofisa ugani katika maeneo yote yanayozalisha zao hilo kuhakikisha wanakuwa jirani na wakulima ili wawafundishe mbinu za kilimo bora na waongeze uzalishaji.

Aliwasisitiza wakulima kuongeza juhudi kwenye kilimo kwa maelezo kuwa kilimo ndio sekta ambayo inaajiri watu wengi zaidi nchini na kwamba serikali imeweka mazingira rafiki ikiwemo kuweka ruzuku kwenye pembejeo.





# Jela miaka 60 kwa kulawiti mtoto

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAHAKAMA ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Vuga, imemhukumu Moh'd Ali Hassan (35) mkazi wa Jumbi Uwandani, Unguja, kutumikia kifungo cha miaka 60 jela.

Moh'd amehukumiwa kifungo hicho baada ya kutiwa hatiani kwa makosa ya kumwingilia mtoto kinyume cha maumbile.

Mshtakiwa huyo alishtakiwa kwa kumwingilia kinyume cha maumbile mtoto wa kike mwenye umri wa miaka sita (jina linahifadhiwa).

Taarifa kutoka mahakamani hapo zilisema mshtakiwa huyo alitenda kosa la kwanza Mei, mwaka huu na kosa la pili Julai 7. mwaka huu, kitendo ambacho ni kinyume cha kifungu namba 133(a) cha Sheria Namba Sita ya mwaka 2018.

**Kesi hiyo ilifunguliwa mahakamani hapo Aprili 24, mwaka huu na mashahidi sita walitoa ushahidi wao mahakamani hapo.**

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Taki Abdulla Habib, alisema mahakama imejiridhisha na ushahidi uliotolewa bila kuwa na chembe ya shaka na kumtia hatiani mshtakiwa kwa makosa hayo.

Kesi hiyo ilifunguliwa Agosti 21, mwaka huu, na mashahidi watano walitoa ushahidi wao mahakamani kujenga msingi wa kesi hiyo.

Katika tukio lingine Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja iliyoko Mahonda, imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka 14 jela Abdi Khamis Mselem (20) na kulipa fidia ya Sh. milioni moja kwa kosa la kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 11 (jina linahifadhiwa).

Mshtakiwa alidai kutenda kosa hilo Machi 6, mwaka huu, kitendo ambacho ni kinyume cha kifungu namba 115(1) na kosa la kutorosha kinyume na kifungu namba 113(1)(b) vya sheria namba 6 mwaka 2018.

Akisoma hukumu, Hakimu Mkazi Luciano Nyengo, alisema Mahakama imejiridhisha na ushahidi uliotolewa ambao hauna chembe ya shaka na kumtia hatiani mshtakiwa kwa makosa hayo.

Kesi hiyo ilifunguliwa mahakamani hapo Aprili 24, mwaka huu na mashahidi sita walitoa ushahidi wao mahakamani hapo.

Wakitoa maoni yao kuhusu hukumu hizo, wanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto Zanzibar, walisema inatia moyo kuona adhabu kali zinatolewa kwa washtakwia wa kesi hizo ili kuwa fundisho kwa watu wengine.

Fatma Khamis Ali alisema adhabu kali kwa makosa hayo zitasaidia kupunguza matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema lazima mmahakama zitoe adhabu kwa mujibu wa sheria na isiwe kosa la ulawiti na ubakaji mahakama moja itatoa adhabu kubwa na nyingine inatoa adhabu ndogo.

Ofisa Miradi wa Kupinga Vitendo vya Udhalilishaji kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Zaina Abdallah Salum, alisema wanapongeza hakumu zinazotolewa kwa baadhi ya mahakama kwa kesi hizo za udhalilishaji ambazo baadhi zinaridhishwa.

## Washauri ukarabati miundombinu korti

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI imeshauriwa kukarabati na kuboresha miundombinu ya mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuwezesha matumizi ya ushahidi wa kielektroniki.

Hatua hiyo imeelezwa itasaidia kuwapo kwa mazingira rafiki kwa wanaotumia mahakama hizo na kuwezesha upatikanaji wa haki katika mazingira bora.

Wadau wa kupinga udhalilishaji Zanzibar, walisema hayo wakati wa mkutano wa kuwasilisha ripoti ya ufanisi wa Mahakama Maalum katika kushughulikia kesi za udhalilishaji tangu kuanzishwa kwake. Mkutano huo uliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wakiwamo Foundation For Civil Society (FCS) na Ubalozi wa Norway.

Kwa mjibu wa ripoti hiyo, kuwa licha ya mahakama hiyo kuonyesha mafanikio makubwa ya usikilizaji wa kesi tangu kuanzishwa kwake, bado miundombinu yake haitoshi kutokana na kukosekana kwa vyombo vya kisasa vya usikilizaji wa kesi, ikiwamo mifumo ya kidigitali (video conference) na ukosefu wa vyumba maalum vya kuwaweka watoto walioathirika na vitendo hivyo.

Hawra Shamte, ambaye ni mtafiti alisema: "Ukosefu wa vifaa katika mahakama na miundombinu duni bado ni changamoto. Mfano majengo za Mahakama ya Vuga, Mahonda, Mkoani na Wete Pemba ni ya zamani na imepitwa na wakati jambo linalosababisha ugumu katika uendeshaji wa kesi hizo."

Aidha, alisema utafiti huo umebaini miongoni mwa mafanikio ya uwepo wa mahakama hiyo ni pamoja na kuongezeka kasi ya usikilizaji wa kesi za udhalilishaji katika mahakama hizo.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo, akisikiliza kero za kinamama wa Kijiji cha Namkulai, kabla ya kuhutubia mkutano wa hadhara kijijini hapo, wilayani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wakulima, mama lishe walia changamoto biashara

Na Mwandishi Wetu

WAKATI mpango wa mabadiliko ya uchumi wa buluu ukifungua mlango wa kukuza uchumi Zanzibar, bado kuna changamoto zimejitokeza kwa wakulima wa mwani na mama lishe kuendesha biashara zao wakati wa mvua.

Hayo yamesemwa kwa nyakati tofauti na wakulima wa mwani na mama lishe katika ukanda wa Paje, Kusini Unguja na katika soko kuu la samaki Malindi mjini Unguja wakati wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya miaka mitatu ya uchumi wa buluu chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mtunza Fedha wa Kikundi cha Furahia Wanawake cha Paje, Sihaba Mustafa Fatawi, alisema mpango wa uchumi wa buluu umewakomboa wakulima wa mwani baada ya kuanza kusarifu zao hilo hatua ambayo imesaidia kuongeza thamani na bei.

Alisema kilo moja ya mwani ambao haujasarifiwa hivi sasa unauzwa Sh. 1,000 wakati uliosarifiwa kilo moja ukiuzwa kwa Sh. 12,000 tangu serikali kuwapatia mashine za kusarifu mwani.

"Bado tuna changamoto kubwa kuhusu matumizi ya fukwe kwa wakulima kutokana na wawekezaji kutuzuia kutumia mita 30 wakati shughuli zetu za uzlaishaji zinategemea fukwe," alisema mkulima huyo.

Alisema wanamshukuru Rais Dk. Mwinyi kwa kuongeza bei ya mwani licha ya kampuni zilizokuwa zikinunua zao hilo kwa bei ya chini kuweka kinyongo. Alisema kuongezeka kwa thamani ya zao hilo katika soko ni dhahiri kwamba Rais Mwinyi amewajali wakulima.

Alisema usarifu wa mwani umewawezesha kuzalisha sabuni, mafuta ya kulainisha ngozi, vipodozi, juisi na unga wa kutengenezea vitafunwa kama keki na biskuti jambo ambalo limewaongezea kipato.

Wakizungumzia matatizo ya soko jipya la samaki la Malindi, mamalishe walisema pamoja na serikali kujenga soko la kisasa lbado hawana shehemu ya kujihifadhi wakati wakitoa huduma kwa kuwa na wakati mgumu kipindi cha mvua na jua.

Asha Saleh Msabaha, alisema mabanda yaliyoezekwa kwa maturubai hayana hadhi na yanaharibu mwonekano wa soko hilo na kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwajengea sehemu maalum ya kutoa huduma za chakula.

Naye Dalali wa soko hilo, Abdaalh Pandu Makame, alisema Rais Dk. Mwinyi wakati anatimiza miaka mitatu ya kukaa madarakani, hawana budi kumpongeza kuwajengea soko la kisasa na kuondoa usumbufu walioukuwa wakiupata wachuuzi wa samaki katika eneo la Malindi na Kinazini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**MAGDALENA FESTO MALITI** anatangaza kupotea kwa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4967-0023** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ALOYSIUS GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015 pia cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0800-0553** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **LOYOLA HIGH SCHOOL** mwaka 2018 na cheti cha chuo chenye usajili namba **TUDOM/2018/01281** kilichotolewa na **THE UNIVERSITY OF DODOMA** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CEN/RB/75520/2023**
**DAR/CEN/RB/75524/2023**
**DAR/CEN/RB/75529/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**OSWIN WENDELINE MAHUNDI** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **TVS KING** yenye usajili namba: **MC 221 CPN** na CHASSIS NAMBA: **MD6M14PA5L4B09499.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SOG/RB/4365/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GS GROUP LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya HAOJUE yenye usajili namba: **MC 443 CFH** na CHASSIS NAMBA: **LC6PCJK23K0015469.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SOG/RB/3426/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 31 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE STANLEY STEPHEN MDOE**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CHRISTOPHER NG'WANYEMI MDOE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 27th day of OCTOBER, 2023.

Dated at DAR ES SALAAM this **27th Day of NOVEMBER, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE DISTRICT

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SINGIDA**
**LILILOPO SINGIDA**
**SHAURI LA ARDHI MAOMBI NA. 83 YA 2020**
**JISURI JISABA............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**NMB BANK PLC............MJIBU MAOMBI NA. 1**
**LJ INTERNATIONAL CO. LTD.........MJIBU MAOMBI NA. 2**
**MWANAIDI HAMISI MDUMA............MJIBU MAOMBI NA. 3**
**MTERY LUKWINYO MBAGA..........MJIBU MAOMBI NA. 4**

**KWA: LJ INTERNATIONAL CO. LTD,**
**MWANAIDI HAMISI MDUMA NA MTERY LUKWINYO MBAGA T/A WEMBELE SHOP ITIGI COMPANY**

**POPOTE ULIPO TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI:**

Kwa kuwa Mwombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa Barazani ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi, ambayo yanaweza kupatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe 07/11/2023.

Mnatakiwa muhudhurie nyinyi au wawakilishi wenu wanaotambulika kisheria siku na saa tajwa hapo juu.

**ANGALIA:** Kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa na kusikilizwa na ikiwa na mjibu maombi namba 1, tu na uamuzi kutolewa bila ya nyinyi au wawakilishi wenu kuwepo.

HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya BARAZA hii leo tarehe 16 Mwezi wa October, Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SINGIDA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa wa GEITA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 45/2023.**
**JINA LA MDAI: SARA ATHUMANI**
**JINA LA MDAIWA: ATHUMANI OTTENO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu za mashauri ya madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: ATHUMANI OTTENO WA MWANZA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**TALAKA/KUACHANA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 16 Mwezi wa 11 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na kupigwa Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 31 Mwezi wa 10 Mwaka 2023.

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA 63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya EMAOI**
**Wilaya ya ARUMERU**
**MADAI NAMBA 11 YA 2023**
**MDAI SELINA ERNEST DULE**
**Ya mdai**
**Mdaiwa AMOS ISACK**
**Kwa AMOS ISACK**
**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)**
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA TAREHE 01/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI KUJIBU MADAI HAYA**

Kwa hiyounahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku JUMATANO tarehe 01/11/2023 saa 4:00 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hatia zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku ilitajwa hapo juu, mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 17/10/2023

HAKIMU MKAZI
EMAOI - ARUMERU

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKLINE EMILIO CHAULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index No. **S3885-0620** kilichotolewa na baraza la Mitihani laTarifa kupitia **WENDA HIGH SCHOOL** mwaka **2020** .Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.


Taarifa ya polisi: **KAT/MPA/RB/256461/2023**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**SALMINI IDDI WAZIRI** anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP YA KIDATO CHA NNE** yenye index namba P1969/0065 iliyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **DUNDA CENTER SECONDARY SCHOOL** mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/PWA/BAG/2124/2023**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**AMOS SIFAEL MGENI** anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP YA KIDATO CHA SITA** yenye index namba **S.1262/0602** iliyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MATEMA BEACH SECONDARY SCHOOL** mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/32520/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Wu_ haiming** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **PHOTON SEMI TALLER** yenye namba za usajili **T834DFS**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/KIG/BUH/806/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**AJIRA T. SHABAN,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. S1261-0002-2010 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari MERRIWA mwaka 2010, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/80953/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya...........TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa...TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na................194/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: FAZLEABBAS BHAIJIBHAI NURBHAI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: MURTAZA FAZLEABBAS BHAIJIBHAI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
ImetolewaleoTarehe ....1... mwezi ...11...mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**
**Piga Simu 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Raia wa kigeni waondoka Gaza, Chile, Bolovia yawaondoa mabalozi

**RAFAH, Misri**

RAIA wa kigeni ambao walikwama wakiwa Ukanda wa Gaza wameanza kuondoka baada ya Misri kufungua mpaka wake wa Rafah.

Hatua hiyo ni ya kwanza kuchukuliwa tangu vita vya Israel dhidi ya Hamas vilipoanza Oktoba 7, mwaka huu.

Kwa mujibu wa chanzo kimoja cha usalama kutoka Misri ni kwamba raia wa kigeni wapatao 500 watavuka mpaka katika kituo cha Rafah wakitokea Gaza na kuingia Misri kuanzia jana.

Picha zilizochukuliwa kutoka eneo hilo zimeonyesha umati wa watu wakiwa upande wa Palestina wakisubiri kuvuka kuingia Misri.

Serikali za mataifa 44 pamoja na mashirika 28 ya Umoja wa Mataifa imewatambua watu wake ambao walikuwa wakiishi Ukanda wa Gaza ambako mashambulizi kutoka majeshi ya Israel yanaendelea.

Mbali na raia hao wa kigeni, pia Wapalestina wapatao 90 waliojeruhiwa vibaya wanatarajia kuvuka mpaka huo kwa ajili ya kupatiwa matibabu nchini Misri.

Jeshi la Israel lilisema kwamba askari wake 11 wameuawa katika mapigano ya ardhini ndani ya Gaza siku ya Jumanne na kufanya idadi jumla ya wanajeshi waliouawa kuwa 326. Askari wengine wawili walijeruhiwa vibaya katika mapigano yaliofanywa Jumanne.

Israel ikidai kuyalenga zaidi ya maeneo 11,000 ya wanamgambo tangu ilipoanza vita vyake dhidi ya Hamas. Katika hotuba yake kwa taifa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu ameahidi kupata ushindi dhidi ya Hamas licha ya athari za kuumiza.

"Tuko kwenye vita vikali. Vitakuwa ni vita vya muda mrefu. Tumekuwa na mafanikio makubwa lakini hasara chungu nzima. Wanajeshi wetu wameanguka katika vita vya haki kabisa, vita dhidi ya nyumba zetu. Na ninaahidi kwa raia wote wa Israel tutafanya kazi hiyo. Tutasonga mbele hadi ushindi," alisema Netanyahu.

Wakati huo huo, Bolivia ilitangaza kukata uhusiano wa kidiplomasia na Israel kutokana na mashambulizi yake katika Ukanda wa Gaza na kuyaita kama fujo na yasiyo na uwiano.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Freddy Mamani, aliwaambia waandishi wa habari kwamba uamuzi wao ni kupinga na kulaani mashambulizi ya kijeshi ya Israel yenye fujo na yasiyo na uwiano yanayotekelezwa Ukanda wa Gaza".

Pia viongozi wa Colombia na Chile wamewaita mabalozi wao walioko nchini Israel kwa majadiliano.

Katika chapisho katika ukurasa wa X, iliyokuwa Twitter, Rais wa Chile Gabriel Boric Fonts alisema nchi yake inalaani vikali ukiukaji usiokubalika wa sheria za kimataifa za kibinadamu unaofanywa na Israel.

Rais wa Colombia, Gustavo Petro aliandika, pia kupitia ukurasa wa X kuwa ikiwa Israeli haitazuia mauaji ya watu wa Palestina hawataweza kuwa nchini humo.

BIDEN NA MFALME ABDULLAH II

Ikulu ya Marekani imetoa maelezo kuhusu mazungumzo ya simu kati ya Rais wa Marekani, Joe Biden na Mfalme Abdullah II wa Jordan.

Viongozi hao wawili walijadili njia za kuharakisha uwasilishaji wa misaada katika eneo hilo linaloendelea kupigwa mabomu.

**DW**



Vifaru vya Israel vikiingia Ukanda wa Gaza kuendesha mapambano na wanamgambo wa Hamas jana. **PICHA: IDF**

# Kiongozi wa mapinduzi jela miaka 12

**BANJUL, Gambia**

KIONGOZI wa mapinduzi yaliyokwama nchini Gambia, Koplo Sanna Fadera, amefungwa gerezani miaka 12 baada ya mahakama kumtia hatiani katika kesi ya uhaini.

Koplo Fadera alituhumiwa kuwa mpangaji mkuu wa njama ya mapinduzi ya kijeshi yaliyotibuliwa Desemba mwaka jana.

Mahakama kuu ilikubaliana kwamba Koplo Fadera alihusika kupanga na kujaribu kupindua serikali iliyochaguliwa kidemokrasia ya Rais Adama Barrow.

Mamlaka ilikuwa imemshtaki Fadera na wanajeshi wengine saba kwa uhaini, kula njama na kuchochea uasi kwa madai ya kuhusika katika jaribio la mapinduzi hayo.

Mahakama iliwaachilia huru maofisa wengine watatu wa kijeshi baada ya kutokutwa na hatia.

Mwanajeshi mwingine ametorka baada ya jaribio la mapinduzi lililoshindwa.

Mahakama pia ilimuachia huru afisa wa polisi na raia wawili waliokuwa wameshtakiwa kwa kuficha taarifa ya uhaini na kula njama ya kutenda uhalifu.

Kabla ya Rais Barrow kuingia madarakani, nchi hiyo ya Afrika Magharibi ilitawaliwa kwa miongo miwili na Yahya Jammeh, ambaye alichukua mamlaka katika mapinduzi ya mwaka 1994, na yeye alizuia majaribio kadhaa ya kutaka kumpindua.

**BBC**

# Mfalme Charles III ashindwa kuomba radhi

**NAIROBI, Kenya**

MFALME Charles III wa Uingereza ameshindwa kuomba radhi kwa maovu yaliyofanywa na utawala wa kikoloni wa nchi yake, licha ya kuonyesha kujutia kutokana na utawala huo nchini Kenya.

Mfalme Charles III yuko nchi Kenya iliingia siku yake ya pili nchini Kenya, ambako aliyatembelea makaburi ya kihistoria ya Kariakor na kuhutubia katika ofisi kuu za Umoja wa Mataifa jijini Nairobi.

Wakati huo mke wake Camilla alilitembelea Shirika la Kuwalinda Wanyama (KSPCA).

Usiku wa kuamkia Jumatano, Mfalme Charles na Camilla walikuwa wageni wa Rais William Ruto kwenye chakula cha jioni katika Ikulu ya Nairobi, mfalme huyo alielezea jinsi Kenya ilivyo na nafasi muhimu katika maisha yake.

Mfalme Charles alisema anasikitika kwa madhila yaliyowafika Wakenya wakati wa kupigania uhuru na kuyataja matendo hayo kuwa ya kukirihisha na yasiyokuwa na haki.

Chini ya utawala wa mama yake, Malkia Elizabeth II, serikali ya Uingereza iliendesha kampeni kali na ya kikatili dhidi ya wapiganiaji uhuru wa vuguvugu la Mau Mau, ambao maelfu waliuawa, kujeruhiwa na kufukuzwa kwenye maeneo yao.

Mfalme Charles licha ya kutoomba radhi, alikiri kuwa hicho kilikuwa kipindi kilicholeta machungu na akaonesha nia ya kutaka kukutana na baadhi ya makundi ya walioathiriwa.

Kwa upande wake, Rais Ruto alisisitiza kuwa yaliyopita si ndwele, lakini ni muhimu kujifunza kutoka kipindi hicho na kuimarisha uhusiano kwa manufaa ya wote.

**BBC**

**Usiku wa kuamkia Jumatano, Mfalme Charles na Camilla walikuwa wageni wa Rais William Ruto kwenye chakula cha jioni katika Ikulu ya Nairobi, mfalme huyo alielezea jinsi Kenya ilivyo na nafasi muhimu katika maisha yake.**

HABARI MICHEZO

# SHIME SASA AGEUKIA MCHEZO KUFUZU WAFCON

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia Twiga Stars juzi ikipata ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wa marudiano wa kufuzu michezo ya olimpiki dhidi ya Botswana, Kocha wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema sasa wanaugeukia mchezo wao wa kufuzu Fainali za Afrika za Wanawake (WAFCON) dhidi ya Togo.

Shime alisema anashukuru kuona amepata matokeo hayo na kusonga mbele kwa jumla ya ushindi wa mabao 3-0 baada ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.

"Niwapongeze wachezaji wangu walipambana na kupata ushindi huu ugenini, walifuata maelekezo vizuri, wapinzani wetu walitumia nguvu na kasi kupiga mipira mirefu lakini tulicheza kwa mipango tuliyojiwekea na kuibua na ushindi huo," alisema Shime na kuongeza;

"Tumefanikiwa kuingia hatua ya tatu na sasa tutakutana na Afrika Kusini, lakini kabla ya kucheza nao tutakuwa na mapumziko mafupi na wachezaji wataenda kwenye majukumu ya klabu zao na mapema mwezi ujao tutajiandaa na mechi ya WAFCON dhidi ya Togo," alisema Shime.

Aliongeza wamepanga kuingia kambini mapema kujiandaa na mchezo dhidi ya Togo na watatumia kambi hiyo kurekebisha mapungufu aliyoyaona kwenye michezo iliyopita.

"Mchezo wa kufuzu Olimpiki umepita, sasa akili zetu tunaelekeza kwenye mchezo wa kufuzu fainali za Afrika, tunataka kupata ushindi ili kusonga mbele," alisema Shime.

Wakati huo huo, mshambuliaji wa timu hiyo, Oppa Clement alisema mechi yao dhidi ya Botswana haikuwa rahisi na walijituma sana kuweza kupata ushindi huo muhimu.

"Kikubwa tumefuata maelekezo ya benchi la ufundi na kupata matokeo mazuri, tunasahau matokeo haya na tunaenda kujipanga kwa mechi ijayo dhidi ya Togo," alisema Oppa.



Vijana wakicheza mpira wa kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nahodha Mtibwa Sugar afunguka kipigo cha KMC

**Na Adam Fungamwango**

KUFUATIA kipigo cha bao 1-0 juzi kutoka kwa KMC, nahodha wa Mtibwa Sugar, Oscar Masai amefunguka juu ya matokeo hayo na kuweka wazi kuwa walizidiwa na wapinzani wao hao na kushindwa kufuata maelekezo ya kocha wao.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Masai alisema wenzao walishinda kutokana na kufanya kila kitu sahihi, ikiwamo kutumia nafasi waliyoipata, hivyo wamekubali matokeo na wanakwenda tena kujipanga kwa ajili ya mechi ijayo.

"Tumepoteza, KMC wameshinda nyumbani tunawapongeza, sisi mipango yetu uwanjani ilifeli, kila tulichofanya hakikufanikiwa, lakini huu ni mpira tumepoteza leo imekwisha tunaangalia mbele, tutaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yetu hadi kila kitu kitakaa sawa," alisema Masai.

Mtibwa ilipoteza mechi hiyo baada ya kushinda mechi yao ya kwanza kwenye Ligi Kuu Alhamisi iliyopita kwa mabao 3-1 dhidi ya Geita Gold, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa kocha Zuberi Katwila ambaye alianza kuifundisha timu hiyo akitokea Ihefu SC.

Awali ilicheza mechi sita bila kupata ushindi wowote, mpaka sasa imecheza mechi nane, ikishinda moja, sare mbili na kupoteza mechi tano na kipigo cha juzi kimesababisha kushuka chini na kukamata mkia ikiwa na pointi tano.

Kwa upande wake, Nahodha wa KMC, Awesu Awesu, alisema wameshinda mchezo huo wa juzi kutokana na mbinu za mwalimu wao, Abdihamid Moalin.

"Mtibwa si timu ya kubeza ila tulistamili nguvu zao, walikosa mabao mengi, sisi tumetumia nafasi," alisema Awesu.

Ushindi huo umeifanya KMC kufikisha pointi 15 na kusogea mpaka nafasi ya tatu (kabla ya mchezo wa jana kati ya Mashujaa FC dhidi ya Azam) mchezo huo ulitarajiwa kuchezwa Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

# Kundemba FC, Uhamiaji ni vita Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu Zanzibar inaendelea tena leo ambapo klabu za Kundemba FC na Uhamiaji zitaumana kwenye Uwanja wa Mau A kukamilisha mzunguko wa tisa wa ligi hiyo.

Mchezo huo unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa kutokana na uhitaji wa kila timu wa pointi tatu muhimu.

Katika mchezo wa leo, Kundemba wana kila sababu ya kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo ili kuondoa jinamizi la kufanya vibaya katika michezo yao mitatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa Kundemba FC, Ali Vuai alisema amekiandaa kikosi chake kucheza kwa kujilinda na kujihami ili waweze kupata matokeo mazuri.

Alisema anajua mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa anacheza na timu yenye uzoefu katika Ligi Kuu, lakini wao hawakupata matokeo mazuri katika mchezo wao uliopita hivyo watakuwa na hamu ya kupata alama atatu.

Alisema katika mchezo huo ameyafanyia kazi mambo kadhaa ambayo yamekuwa yakisababisha kutopata matokeo mazuri katika michezo waliyocheza.

Alisema miongoni mwa mambo hayo ni kuinoa safu ya ulinzi ambayo imekuwa ikiruhusu magoli mengi lakini pia kuhakikisha mabeki wa kushoto kufanya kazi yao kulingana na mfumo wa kocha huyo.

"Tunaendelea kusahihisha makosa ambayo mara kwa mara tunayaona katika michezo mingi tuliyocheza, naaamini makosa hayo tukiyaweka sawa basi timu itaweza kufanya vizuri," alisema Kundemba.

Aidha, kocha huyo amewaomba mashabiki wa timu hiyo kuendelea kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwapa hamasa na kuwatia moyo wachezaji wake waweze kufanya vizuri.

"Mashabiki wetu wasivunjike moyo kwa matokeo ambayo tumeyapata, wao ni muhimu kwetu hasa katika mpango wetu huu wa kuhakikisha tunafanya vizuri katika mchezo huu na inayofuata," alisema Vuai.

Kundemba FC ipo nafasi ya 10 katika msimamo wa Ligi kuu ya Zanzibar ikiwa na alama 9 ikishinda michezo miwili, sare tatu pamoja, imefungwa michezo mitatu wakati wapinzani wao wa leo wapo katika nafasi ya nane wakiwa na pointi 11.

## ZISIKUPITE

### BISSAKA MAMBO MAGUMU

MAZUNGUMZO kati ya Manchester United na beki wao Aaron Wan-Bissaka kuhusu mkataba mpya yanaonekana kukwama. United sasa wanafikiria kutumia kifungu cha nyongeza ya miezi 12 katika mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. **(Daily Mail)**

### TREVOH ATAKIWA MAN U

KLABU ya Manchester United inapania kumnunua mlinzi wa Chelsea Trevoh Chalobah, huku Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 24 akiambiwa kuwa hayumo katika mipango ya Mauricio Pochettino. **(Teamtalk)**

### TONEY KUUZWA

KLABU ya Brentford iko tayari kumuuza Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, mwezi Januari na wameweka bei ya pauni milioni 80 kwa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England. **(Evening Standard)**

### RENSCH ANYATIWA

LIVERPOOL inamnyatia mlinzi wa Ajax, Devyne Rensch mwenye umri wa miaka 20, lakini wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi. **(Football Insider)**

### LEONARDO ATAKIWA

KLABU ya Newcastle United imeanza mazungumzo na Santos kuhusu usajili wa mshambuliaji wa Brazil, Marcos Leonardo mwenye umri wa miaka 20, ambaye anakadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 25 **(UOL).**

### ARIAS AWANIWA

KLABU za Wolves, West Ham na Leeds United zinamwania winga wa Fluminense na Colombia, Jhon Arias mwenye umri wa miaka 26. **(Teamtalk)**

### COSTA AWINDWA MAN U

KLABU ya Manchester United ilituma maskauti kumtazama mlinda mlango wa Ureno Diogo Costa mwenye umri wa miaka 24, akiichezea Porto dhidi ya Vizela siku ya Jumapili. **(A Bola)**

### RAZI AGOMBEWA

ARSENAL, Chelsea na Real Madrid zinawania kumsajili winga wa Ireland, Naj Razi mwenye umri wa miaka 17 kutoka Shamrock Rovers. **(Sun)**

### RODRYGO MKATABA MPYA

WINGA wa Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 22 anatazamiwa kusaini mkataba mpya na Real Madrid hadi 2028, licha ya kuhusishwa na klabu za Liverpool na Paris St-Germain. **(Fabrizio Romano)**

### FATI ATAKIWA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 21, ambaye yuko Brighton kwa mkopo, anazivutia klabu za Saudi Arabia. **(Estadio Deportivo)**

### GNONTO AWANIWA

KLABU ya Everton iko tayari kuchuana na Roma na Lazio kwa ajili ya kuinasa saini ya winga wa Italia, Wilfried Gnonto mwenye umri wa miaka 19, ambaye alijaribu kulazimisha kuondoka Leeds msimu wa joto. **(Teamtalk)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ROMA KUMBAKIZA ROMELU LUKAKU

## Yaandaa mpango wakubadilishana wachezaji na Chelsea, kwa kumtoa...

**ROME, Italia**

AS Roma imepanga kufanya mabadilishano ya wachezaji na Klabu ya Chelsea kwa kuwapa Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 26, ili kumsainisha mkataba wa kudumu Romelu Lukaku wakati wa dirisha lijalo la majira ya joto.

Roma inahitaji kumsainisha mkataba wa kudumu Lukaku kwa sababu imevutiwa na kiwango chake tangu ajiunge nao katika dirisha lililopita. Ripoti zinadai Abraham anataka kuondoka mwisho wa msimu huu wakati ambao kocha Jose Mourinho pia anatarajiwa kuondoka na ripoti zikimhusisha na kuwa kwenye mpango wa kutimkia nchini Hispania, England na Saudi Arabia.

Tammy mwenyewe anadaiwa kutamani kuondoka ili kubadilisha mazingira na kupata changamoto mpya baada ya kutofanya vizuri msimu uliopita na alifunga mabao tisa tu tofauti na msimu wake wa kwanza alifunga mabao 27 kwenye mechi 53.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England tangu uanze msimu huu hajacheza mechi hata moja kutokana na majeraha ya goti yanayomwandama ambayo anatarajiwa kupona mwakani, mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwaka 2026.

# WENGER AIPA UBINGWA TOTTENHAM

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, anaamini Tottenham Hotspur italeta ushindani mkubwa na itakuwa moja ya timu yenye uwezo wa kubeba ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Spurs ambayo imezaliwa upya chini ya kocha mpya Ange Postecoglou, ipo kileleni kwenye msimamo baada ya kucheza mechi 10.

Inaongoza kwa pointi mbili mbele ya wapinzani wao wa Jiji moja Arsenal kwa kushinda mara nane na kutoka sare mbili kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Siku zote napenda kusema kile ninachohisi," alisema Wenger akinukuliwa na beIN Sports.

"Kwa undani, ninaamini Tottenham itakuwa moja kati ya timu inayogombea ubingwa wa ligi msimu huu. Walimnunua James Maddison, ambaye ni mchezaji mzuri, yeye ndiye kiungo wa kutokea chini hadi kiungo cha juu na ameongeza ubunifu wa kiufundi kwenye timu.

"Pia walimnunua Micky Van de Ven, ambaye namuona ni mchezaji wa kipekee kabisa, walikuwa na udhaifu kwenye nafasi ya kipa kwani msimu uliopita kipa Hugo Lloris hakuwa na misimu bora, kiwango chao kuanzia kati kwenye safu ya kiungo ipo vizuri kwa sasa," alisema Wenger.

Hata hivyo, Wenger anaamini timu kadhaa pia zipo katika kinyang'anyiro cha kuwania ubingwa msimu huu,

"Msimu huu naweza kuitaja Arsenal kwa ajili yangu, Liverpool, Tottenham, Manchester City bila shaka wapo kwenye msafara huo," aliongeza.

Arsenal, Liverpool ziliibuka na ushindi kwenye mechi zao mwishoni mwa juma lililopita, huku Manchester City ikiichapa Manchester United mabao 3-0.

Arsenal ilibamiza Sheffield United mabao 5-0, Liverpool ikiondoka na ushindi wa mabao 3-0 ilipomenyana dhidi ya Nottingham Forest.



# Saudi Arabia kuandaa Kombe la Dunia 2034

**NYON, Uswisi**

SAUDI Arabia ndiyo nchi pekee iliyowasilisha ombi la kuandaa Kombe la Dunia la FIFA 2034, Shirikisho hilo la soka la kimataifa, limethibitisha.

FIFA ilikuwa imealika ofa kutoka bara la Asia na Oceania kwa ajili ya michuano hiyo kufikia Jumanne na Saudi Arabia ilitangaza kuwa ingejitosa dakika chache baada ya tangazo hilo Oktoba 4.

Australia ilisema Jumanne haitawasilisha ombi la kuandaa mashindano hayo na kuiacha Saudi Arabia kama mgombea pekee.

"Kama ilivyowekwa katika kanuni za zabuni zilizoidhinishwa na Baraza la FIFA, utawala wa FIFA utafanya michakato ya kina ya zabuni na tathmini kwa matoleo ya 2030 na 2034 ya Kombe la Dunia la FIFA na wenyeji watakaoteuliwa na mabaraza ya Shirikisho hilo yanatarajiwa kufanyika mwaka 2024," FIFA ilisema.

FIFA pia ilithibitisha kwamba uthibitisho pekee wa nia ya kuandaa Kombe la Dunia la 2030 ulitoka kwa Morocco, Ureno na Hispania huku Uruguay, Argentina na Paraguay zikiandaa michezo ya kusherehekea.

FIFA bado inahitaji kuipigia chapa Saudi Arabia kama mwenyeji uamuzi ambao huenda ukafanywa mwishoni mwa mwaka ujao lakini hiyo inaonekana kuwa rasmi.

Mpango wa matumizi ya fedha za michezo nchini Saudi Arabia ulioidhinishwa na Mwanamfalme wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman umeelezwa kuwa ni kutumia michezo ili kulainisha sura ya taifa ambayo mara nyingi huhusishwa na rekodi yake kuhusu haki za wanawake na mauaji ya mwaka 2018 ya mwandishi wa habari Jamal Khashoggi.

Rais wa FIFA, Gianni Infantino, amejenga uhusiano wa karibu na soka la Saudia na mwana mfalme binafsi, na ameonekana kwa muda mrefu akijaribu kuongoza mashindano ya Shirikisho la Soka Duniani kuelekea ufalme huo.

Wakati FIFA ilipofanya makubaliano mwezi huu kuwa na ofa moja pekee ya kuwa mwenyeji wa Kombe la Dunia la 2030, kuunganisha Hispania, Ureno na Morocco na mechi tatu zilizowekwa Amerika Kusini - pia ilifuatilia kwa haraka mbio za kuandaa mwaka 2034 na mashirikisho ya wanachama pekee barani Asia na Oceania imetimiza masharti ya kutoa zabuni.

# Drinkwater atundika daluga

**LONDON, England**

MCHEZAJI wa zamani wa Leciester City, Danny Drinkwater, amestaafu soka akiwa na umri wa miaka 33 kwa sababu ya kukosa timu ya kuichezea.

Drinkwater alikosa timu ya kukipiga tangu alipotemwa na Chelsea Julai mwaka jana na sasa ameamua kustaafu.

"Napenda kutangaza rasmi nimestaafu rasmi soka la kulipwa. Ilikuwa muda mrefu sana hususan mwaka jana, lakini muda umefika wa kutoa taarifa.

"Sidhani kama itanisumbua kusema kwa sababu nimejiandaa nilisubiri sana nipate nafasi ya kucheza lakini haikuwezekana," alisema Drinkwater.

Drinkwater alitokea Manchester United kabla ya kutolewa kwa mkopo mara kadhaa kwenye timu za Ligi Daraja la Kwanza kabla ya kuibukia Leicester mwaka 2016.

Akiwa Leicester alitengeneza jina lake, alipocheza michezo 218 na kubeba ubingwa wa Ligi Kuu England mwaka 2016.

Mafanikio ya Drinkwater yalimhakikishia uhamisho wa pauni milioni 35, lakini msimu wake wa kwanza Chelsea alikumbwa na majeraha na kucheza mechi 12 tu za ligi.

Drinkwater ambaye aliichezea Timu ya Taifa ya England mara tatu baada ya hapo hakujumishwa katika kikosi cha Chelsea baadaye akatolewa kwa mkopo Burnley, Aston Villa, Kasimpa ya Uturuki na hatimaye Reading kabla ya mkataba wake kumalizika Chelsea Juni mwaka jana.

Drinkwater alifichua siri kwamba kabla ya kustaafu alikuwa na matumaini ya kuhamia Saudi Arabia na pia kukiri alikuwa tayari kurejea tena Leicester.



# KOCHA MINZIRO AIPANGIA MIKAKATI KAGERA SUGAR

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa Tanzania Prisons, Fred Felix 'Minziro', amesema ameshafanyia kazi upungufu katika timu yake kwa mchezo wao wa kesho dhidi ya Kagera Sugar.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka mkoani Kagera, Minziro alisema moja ya maeneo ambayo ameyafanyia kazi ni safu yake ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikikosa magoli mengi licha ya nafasi nyingi kutengenezwa.

Alisema amefanyia kazi na anaamini ataanza kuona matunda yake kwenye mchezo wa kesho utakaochezwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba.

"Safu yangu ya umaliziaji ilikuwa na upungufu ambao ulitugharimu kwenye michezo iliyopita tukashindwa kupata matokeo, nimeanza kufanyia kazi na naamini kwenye mchezo wetu wa Ijumaa (kesho) nitaanza kuona mabadiliko kwenye safu yangu ya ushambuliaji," alisema Minziro.

Kocha huyo alisema lengo lake ni kupata pointi tatu katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa.

Alisema anaiheshimu Kagera Sugar kwani ina wachezaji wazuri na amewataka wachezaji wake kuingia kwa tahadhari kwenye mchezo huo.

Alisema leo jioni watafanya mazoezi yao ya mwisho kuweka mambo sawa ndani ya kikosi chake tayari kwa mchezo huo wa ugenini.

Tanzania Prisons mchezo wao uliopita dhidi ya Geita Gold uliochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya ulimalizika bila kufungana.

## Kuogelea Taifa kukutana IST

**Na Shufaa Lyimo**

VIONGOZI, benchi la ufundi na wachezaji wa timu ya taifa ya mchezo wa kuogelea watakutana Jumamosi katika Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) kujadili kwa pamoja ushiriki wa timu katika mashindano ya kanda ya tatu ya Afrika.

Mashindano hayo yatakayohusisha nchi mbalimbali za Afrika yamepangwa kufanyika Novemba 21-24 nchini Rwanda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Michel Livingstone alisema lengo la kikao hicho ni kupanga mikakati ya namna gani watashiriki mashindano hayo huku pia kuwekana wazi aina ya mtindo wa kuogelea watakaoenda kushiriki.

"Tutakutana na wachezaji Jumamosi na kumweleza kila mmoja mtindo atakaokwenda kuutumia tutakapokuwa katika mashindano hayo ambayo tutatumia mabwawa ya mita 25, ni lazima kujiandaa mapema," alisema Livingstone.

Aidha, alisema wachezaji hao walishaanza maandalizi muda mrefu kwa kutumia mitindo mbalimbali.

"Malengo yetu kupata ubingwa kwenye mashindano hayo, tuna imani na wachezaji tulionao watafanya vizuri, kukutana kwetu Jumamosi pia ni kwa ajili ya viongozi wetu kuwapa hamasa wachezaji kwenye wakati huu wa maandalizi," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa wachezaji wanafanya mazoezi ya pamoja wakitokea nyumbani wakisubiri kuingia kambini wiki moja kabla ya kuanza safari kuelekea Rwanda.

Timu hiyo ina jumla ya wachezaji 30 kutoka klabu mbalimbali za Tanzania Bara ambao wamekidhi vigezo vya kushiriki.




Mchezaji wa Timu ya Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), Said Issa (mwenye jezi ya bluu), akimiliki mpira huku akizongwa na mchezaji wa Chuo cha Biashara (CBE), Patrick John, katika mchezo wa kirafiki uliochezwa viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba, Yanga hatari hapa

INATOKA UK. 24

mtindo huo.

Fabrice Ngoma ndiye aliyeifungia Simba bao kwa kichwa katika mechi ya ufunguzi, Simba ilipoifunga dhidi ya Mtibwa Sugar na kupata ushindi wa mabao 4-2, mechi iliyochezwa Agosti 15, mwaka huu na upande wa Yanga aliyefunga ni Nzengeli, Ijumaa iliyopita, Yanga ilipoifunga Singida Fountain Gate mabao 2-0.

Takwimu zetu zinaonyesha katika ya mabao 16 ambayo Simba imefunga, 11 yamefungwa kwa mguu wa kulia, manne kwa mguu wa kushoto, huku Clatous Chama akifunga mabao mawili kutumia wa kushoto, moja Willy Onana na lingine Moses Phiri 'Jenerali'.

Kwa upande wa Yanga yenyewe imepachika nyavuni mabao 20 mpaka sasa, 16 yakifungwa mguu wa kulia na manne kwa mguu wa kushoto, ambayo matatu pekee yamefungwa na Aziz Ki, moja likiwekwa wavuni na Mkongomani Nzengeli.

## Tanzania, Yanga zawania tuzo CAF

INATOKA UK. 24

ASEC Mimosas (Ivory Coast), Al Ahly (Misri), Raja Club Athletic na Wydad Athletic Club za Morocco.

Timu nyingine ni Mamelodi Sundowns, Marumo Gallants (Afrika Kusini) na vigogo wa Tunisia, Esperance de Tunis.

Wachezaji wanaume wanaowania Tuzo ya Golikipa Bora ni Djigui Diarra wa Yanga, Mohamed ElShenawy (Al Ahly), Yassine Bounou nyota wa Morocco anayekipiga Al Hilal, Andre Onana (Cameroon- Manchester United), Ronwen Williams (Afrika Kusini-Mamelodi Sundowns) na Edouard Mendy (Senegal na Al Ahli).

Makipa wengine ni Oussama Benbot (Algeria- USM Alger), Youssef El Motie (Morocco- Wydad Athletic Club), Pape Mamadou Sy (Senegal -Generation Foot) na Landing Badji (Senegal-AS Pikine), Yahia Attiyat Allah, Yahya Jabrane, Youssef El Motie (Morocco - Wydad), Peter Shalulile (Namibia - Mamelodi Sundowns), Percy Tau (Afrika Kusini-Al Ahly), Ranga Chivaviro (Afrika Kusini- Marumo Gallants/Kaizer Chiefs), Ronwen Williams (Mamelodi Sundowns), Ali Maaloul (Tunisia -Al Ahly) na Mohamed Ali Ben Romdhane ambaye sasa anaichezea Ferencvaros.

Tuzo ya Mchezaji Chipukizi inawaniwa na Dango Ouattara raia wa Burkina Faso anayecheza Bournemouth, Souleymane Alio (Burkina Faso -New Stars), Ernest Nuamah (Ghana - Olympique Lyonnais), Abdessamad Ezzalzouli (Morocco -Betis), Bilal El Khannous (Morocco - Genk), Gift Orban (Nigeria - KAA Gent), Lamine Camara (Senegal -Generation Foot/Metz), Pape Amadou Diallo (Senegal -Generation Foot/Metz), Pape Demba Diop (Senegal -Zulte Waregem) na Amara Diouf (Senegal - Generation Foot).

Tuzo ya Kocha Bora wa mwaka inawaniwa na Abdelhak Benchikha wa USM Alger, Marcel Koller (Al Ahly), Juan Micha Obiang (Equatorial Guinea), Tom Saintfiet (Gambia), Baciro Cande (Guinea Bissau), Amir Abdou (Mauritania), Walid Regragui (Morocco), Chiquinho Conde (Msumbiji), Aliou Cisse (Senegal) na Pape Thiaw aliyeipa Senegal ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

# Michezo

Alhamisi Novemba 2, 2023

Nipashe



## Roma kumbakiza Lukaku

UKURASA 21




Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Obinna Anyalebenchi (wa tatu kushoto), akibadilishana nyaraka na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, baada ya kusaini mkataba wa udhamini wenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Sheria wa SBL, Lucia Minde (wa pili kushoto) na (wa pili kulia) ni Wakili wa Simba, Hosea Chamba. **PICHA: JOHN BADI**

# SIMBA, YANGA HATARI HAPA

●●●Kila upande unatakiwa kuongeza umakini ili kuepuka...




**Na Adam Fungamwango**

WAKATI homa ya mechi ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga ikizidi kupanda takwimu zinaonyesha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao ni hatari kwa mashuti ya nje ya eneo la hatari kuliko wapinzani wao ambao wako imara kwenye idara ya kupiga mipira ya faulo, imefahamika.

Simba inatarajia kuikaribisha Yanga katika mechi ya mzunguko wa kwanza itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, Yanga ina uwiano mzuri wa mabao ya nje ya eneo la hatari kuliko Simba ambao wao mabao yao mengi wamefunga wakiwa ndani ya boksi.

Yanga ambayo inakwenda kucheza dhidi ya Simba ikiwa na mabao 20, sita imeyafunga ikiwa nje ya boksi na matatu kati ya hayo yamewekwa wavuni na Stephane Aziz Ki huku Maxi Nzengeli, Yao Kouassi na Mudathir Yahaya kila mmoja akifunga bao moja kwa mashuti ya nje ya eneo la hatari.

Wakati Yanga ikiwa na mabao sita ya nje ya bosi, Wekundu wa Msimbazi wao wamefunga mabao mawili tu kati ya 16 iliyoyaweka wavuni mpaka sasa.

Magoli ya Simba yamefungwa na Saido Ntibazonkiza kwenye mechi dhidi ya Singida Fountain Gate, ikipata ushindi wa mabao 2-1 na lingine likiwekwa wavuni na Jean Baleke, Jumamosi iliyopita ilipopata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu SC kutoka Mbeya.

Mechi hiyo inakwenda kuchezwa huku Yanga ikiwa ni tishio linapokuja suala ya mipira ya faulo, tayari wana mabao mawili iliyofunga kwa mtindo huo, yote yakiwekwa wavuni na Aziz Ki katika mechi dhidi ya JKT Tanzania wakishinda 5-0 na dhidi ya Azam FC, ikishinda mabao 3-2, Simba ikiwa haina bao lolote kwa adhabu ndogo mpaka sasa.

Hata hivyo, Simba inaonekana ni timu inayowalazimisha wapinzani wake kufanya madhambi katika eneo la hatari kwa sababu imepata penalti mbili mpaka sasa na zote imezitumia kupitia kwa Saido, akifunga kwenye mechi dhidi ya Prisons timu yake ikishinda mabao 3-1, Baleke akifanya hivyo katika mechi dhidi ya Coastal Union, ikishinda mabao 3-0.

Timu zote mbili zinaonekana bado zina matatizo kufunga mabao ya vichwa kwani kila timu ina bao moja tu lililofungwa kwa

INAENDELEA UK. 23

## Tanzania, Yanga zawania tuzo CAF

**CAIRO, Misri**

TIMU ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), pamoja na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wametajwa kuwania tuzo za Shirikisho la Soka Afrika (CAF) ambazo zimepangwa kufanyika Desemba 11, mwaka huu jijini Marrakech, Morocco, imefahamika.

Mafanikio makubwa ya Taifa Stars mwaka huu ni kukata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2024), zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye kundi lake kwa kulazimisha sare ya ugenini dhidi ya vinara, Algeria.

CAF imetoa orodha hiyo ya awali kufuatia mafanikio ya timu hizo katika kipindi cha kuanzia Novemba, mwaka jana hadi Septemba, mwaka huu.

Mataifa mengine yanayowania tuzo hizo zinazotolewa kila mwaka na CAF ni pamoja na Cape Verde, Gambia, Guinea Bissau, Equatorial Guinea, Mauritania, Morocco, Msumbiji, Namibia na Senegal.

Mbali na Yanga ambayo msimu uliopita ilifanikiwa kucheza fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, klabu nyingine zinazowania tuzo ya Klabu Bora ni CR Belouizdad, USM Alger zote za Algeria,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >